ISSN 0856 - 034X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

***Supplement No. 14*** ***21st April, 2023***

***SUBSIDIARY LEGISLATION***

*To The Gazette of the United Republic of Tanzania No. 14 Vol. 104 Dated 21st April, 2023*
Printed by The Government Printer, Dodoma by Order of Government

GOVERNMENT NOTICE NO. 287 published on. 21/4/2023

SHERIA YA AFYA NA USALAMA MAHALI PA KAZI,
(SURA YA 297)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 109)*

KANUNI ZA MATUMIZI YA MADINI YA RISASI ZA MWAKA 2023

## MPANGILIO WA KANUNI

*Kanuni* *Jina*

1. Jina.
2. Tafsiri.
3. Matumizi.
4. Taarifa kuhusu mafunzo.
5. Wajibu wa watu wanaoweza kukumbwa na madini ya risasi.
6. Tathmini ya uwezekano wa kukumbwa na madiniya risasi.
7. Ufuatiliaji wa afya.
8. Ukanda wa kuvaa kifaa kinga cha kupumulia.
9. Kumbukumbu.
10. Udhibiti wa kukumbwa na madini ya risasi.
11. Vifaa kinga.
12. Usafi wa majengo na mitambo.
13. Kudumisha hatua za udhibiti.
14. Kuweka lebo, ufungaji, usafirishaji na uhifadhi.
15. Mazuio.

SHERIA YA AFYA NA USALAMA MAHALI PA KAZI,
(SURA YA 297)

---

## KANUNI

---

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 109)*

KANUNI ZA MATUMIZI YA MADINI YA RISASI ZA MWAKA 2023

Jina

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Matumizi ya Madini ya Risasi za Mwaka 2023.

Tafsiri

2. Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"madini ya risasi" maana yake ni madini ya risasi, mchanganyiko wa vitu na madini ya risasi na viambata vya madini ya risasi ambavyo vinaweza kufyonzwa kwa njia yeyote na binadamu;

"Mamlaka ya Ukaguzi iliyoidhinishwa" maana yake ni Mamlaka ya Ukaguzi iliyoidhinishwa kwa ajili ya-

(a) ufuatiliaji wa viwango vya madini ya risasi katika hewa, au

(b) uchambuzi wa viwango vya madini ya risasi katika damu au mkojo;

"rangi yenye madini ya risasi" maana yake ni rangi yoyote yenye madini ya risasi inayoweza kupulizwa, kupakwa au kubandikwa;

Sura 297

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Afya na Usalama Mahali Pa Kazi;

"mamlaka" maana yake ni Mamlaka ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi;

"tetra-alkyl" maana yake ni kiambata cha kemikali kwenye madini ya risasi;

"ufuatiliaji wa kibaiolojia" maana yake ni kupima kiwango cha madini ya risasi kwenye damu au mkojo;

"vifaa kinga vya kupumulia" maana yake ni kifaa

ambacho huvaliwa angalau mdomoni na puani ili kuzuia kuvuta hewa ambayo si salama, na ambacho kimeidhinishwa na Mamlaka; na

"viwango vya afya na usalama" maana yake ni viwango vya afya na usalama kama vilivyoainishwa chini ya Kanuni hizi.

Matumizi

3. Kanuni hizi zitatumika kwa kila mwajiri na mtu aliyejiajiri ambapo madini ya risasi yanazalishwa, yanachakatwa, yanatumiwa, yanashikwa au kuhifadhiwa katika hali ambayo inaweza kuvutwa, kumezwa au kufyonzwa na mtu yeyote katika sehemu hiyo ya kazi.

Taarifa kuhusu mafunzo

4.-(1) Mwajiri yoyote anayejihusisha na kazi zinazohusiana na madini ya risasi baada ya kushauriana na Kamati ya Afya na Usalama iliyoundwa, atatakiwa kuwapa wafanyakazi taarifa na mafunzo kuhusiana na-

(a) vyanzo vinavyoweza kusababisha kukumbwa na madini ya risasi;

(b) hatari ya kiafya inayoweza kusababishwa na kukumbwa na madini ya risasi, ikijumuisha hatari za kiafya kwa familia za wafanyakazi na wengine, ambao wanaweza kuathirika kutokana na vifaa au nguo zilizotumika kazini kupelekwa nyumbani;

(c) tahadhari zinazopaswa kuchukuliwa na mfanyakazi kumkinga dhidi ya hatari za kiafya zinazotokana na kukumbwa na madini ya risasi, ambazo zinajumuisha kuvaa na kutumia vifaa kinga;

(d) umuhimu, matumizi sahihi, matunzo na uwezo wa vifaa kinga, vifaa na hatua za udhibiti wa uhandisi zinazotolewa;

(e) tathmini ya kukumbwa na madini ya risasi, madhumuni ya kuchukua sampuli za hewa, umuhimu wa ufuatiliaji wa afya za wafanyakazi na faida za muda mrefu za kufanyiwa ufuatiliaji wa kiafya;

(f) muda wa kazi na kiwango cha ukomo wa kukumbwa na madini ya risasi;

(g) taratibu salama za ufanyaji kazi kuhusu utumiaji, utunzaji, usindikaji, uhifadhi na utupaji wa kitu au bidhaa yoyote iliyo na madini ya risasi, ili kupunguza uenezaji wa madini ya risasi nje ya eneo la kazi; na
(h) taratibu zinazopaswa kufuatwa katika tukio la kusambaa kwa madini ya risasi au dharura nyingine yoyote.

(2) Mafunzo ya rejea yatatolewa kuhusu masuala yanayokusudiwa katika kanuni ndogo ya (1) angalau kila mwaka au mkaguzi atakavyoelekeza.

(3) Mafunzo yatatolewa na mtu ambaye ana weledi na anayetambuliwa na Mamlaka kutoa mafunzo hayo.

(4) Mwajiri au mtu aliyejiajiri atahakikisha kwamba anatoa taarifa na maelekezo yanayohusiana na kukumbwa na madhara ya madini ya risasi kwa mtu yeyote atakayefika katika eneo lake la kazi.

(5) Mwajiri atatoa maelekezo kwa maandishi ya taratibu zinazokusudiwa katika kanuni ndogo ya (1)(h) kwa madereva wa magari yanayobeba madini ya risasi ambayo yana uwezekano wa kusababisha uchafuzi wa mazingira au kuleta athari kwa watu.

Wajibu wa watu wanaoweza kukumbwa na madini ya risasi

5. Mtu yeyote ambaye amekumbwa au anayeweza kukumbwa na madini ya risasi mahali pa kazi, atatii maagizo yoyote halali yanayotolewa na mwajiri au mwakilishi wake au mtu aliyejiajiri, kuhusu-
(a) kuvaa na kutumia vifaa kinga;
(b) uvaaji wa vifaa vya ufuatiliaji ili kupima kiwango cha kukumbwa na madini ya risasi kilichopo katika hewa;
(c) mpangilio wa mazingira ya kazi, usafi binafsi na taratibu za utunzaji afya na mazingira; na
(d) mafunzo na maelekezo yaliyotolewa kama ilivyokusudiwa katika kanuni ya 4.

Tathmini ya uwezekano wa kukumbwa na madini ya risasi

6.-(1) Mwajiri au mtu aliyejiajiri atahakikisha kwamba -
(a) tathmini ya uwezekano wa kukumbwa na

madini ya risasi katika eneo la kazi inafanywa na mamlaka iliyoidhinishwa, ili kubaini kama mtu yeyote anaweza kuwa katika hatari ya kukumbwa na madini ya risasi; na

(b) taarifa ya tathmini iliyotajwa katika kanuni ndogo ya 1(a) itawasilishwa kwa Mkaguzi Mkuu.

(2) Mwajiri kabla ya kufanya tathmini, atashauriana na Kamati ya Afya na Usalama ili kuweka utaratibu wa kufanya tathmini ya uwezekano wa kukumbwa na madini ya risasi.

(3) Wakati wa kufanya tathmini inayokusudiwa katika kanuni ndogo ya (1) mwajiri au mtu aliyejiajiri atazingatia -

(a) uwepo wa madini ya risasi ambayo mtu anaweza kukumbwa nayo;

(b) mahali yalipo, muundo wa madini ya risasi na kiwango ambacho mtu anaweza kukumbwa nacho;

(c) kazi zinazofanyika na uwezekano wa kushindwa kwa hatua za udhibiti; na

(d) maelezo ya kukumbwa yanayotarajiwa -

(i) kama madhara ni juu ya kikomo cha kukumbwa na madini ya risasi, ilikuweza kuchagua vifaa kinga sahihi vya kupumulia wakati hatua za udhibiti wa kihandisi ukisubiriwa;

(ii) endapo kukumbwa na madini ya risasi kama hayo ni ya nyakati tofauti, mzunguko wa kujirudia na muda wa kukumbwa;

(iii) idadi ya wafanyakazi waliopo katika mazingira ya kukumbwa na madini ya risasi na mtu mwingine yeyote ambaye anaweza kuwa katika mazingira hayo; na

(iv) pale inapohitajika, matokeo ya ufuatiliaji wa awali wa madini ya risasi uliofanyika mahali pa kazi yanapatikana.

(e) hatua zinazopaswa kuchukuliwa ili kupunguza kukumbwa na madini ya risasi katika kiwango cha chini kabisa kinachowezekana na hatua zinazopaswa kuchukuliwa ili kupunguza viambata hewa vya madini ya risasi kwenda kwenye mazingira;

(f) taratibu za kushughulikia dharura; na

(g) taratibu za uondoaji wa taka zenye madini ya risasi kutoka mahali pa kazi.

(4) Pale ambapo tathmini au mapitio ya tathmini yaliyofanyika kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1) na (5) yanaonesha kwamba, mtu yeyote anaweza kukumbwa na madini ya risasi, mwajiri au mtu aliyejiajiri atahakikisha kwamba kukumbwa kunadhibitiwa kama inavyoelekezwa katika kanuni ya 11.

(5) Mwajiri au mtu aliyejiajiri atapitia tathmini iliyowekwa katika kanuni ndogo ya (1) endapo -

(a) kuna sababu ya kuamini kwamba tathmini ya awali haifai tena;

(b) hatua za udhibiti hazina ufanisi tena;

(c) maendeleo ya kiteknolojia au kisayansi yanaruhusu mbinu bora zaidi za udhibiti; au

(d) kumekuwa na mabadiliko makubwa katika-

(i) taratibu za kufanya kazi;

(ii) aina ya kazi iliyofanywa; au

(iii) aina ya vifaa kinga vinavyotumika kudhibiti kukumbwa na kanuni ndogo za (2) na (3) zitatumika.

Ufuatiliaji wa afya

7. (1)Mwajiri atahakikisha kwamba mfanyakazi anakuwa chini ya ufuatiliaji wa afya wa mkaguzi wa afya mahali pa kazi ikiwa -

(a) mfanyakazi amekumbwa na viambata hewa vya madini ya risasi kwa kiwango zaidi ya kikomo cha kukumbwa na madini ya risasi kazini;

(b) mfanyakazi amekumbwa na madini ya risasi ya tetra-alkyl; na

(c) mkaguzi wa afya aliyeidhinishwa amethibitisha kwamba mfanyakazi husika

anapaswa kuwa chini ya ufuatiliji wa afya.

(2) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (1), mwajiri atahakikisha kwamba-

(a) uchunguzi wa awali wa afya unafanyika mara tu, au ndani ya siku kumi na nne baada ya mtu kuanza kazi;

(b) kuzingatia kanuni ndogo ya (2)(a) pale ambapo madini ya risasi tofauti na madini ya risasi ya tetra-alkyl yanahusika, kipimo cha madini ya risasi ya damu ya mfanyakazi na kiwango cha hemoglobini kitafanyika kama ilivyoainishwa katika Sehemu A ya Jedwali;

(c) kipimo cha haraka cha mkusanyiko wa madini ya risasi kwenye mkojo kwa wafanyakazi waliokumbwa na madini ya risasi yenye tetra-alkyl na baada ya hapo kwa vipindi kama ilivyoainishwa katika Sehemu B ya Jedwali; na

(d) uchunguzi wa afya na vipimo vya kibaiolojia vya afya husika vitafanyika kwa kuzingatia maelekezo ya mkaguzi wa afya mahali pa kazi aliyeidhinishwa.

(3) Mwajiri atahakikisha kuwa hakuna mwajiriwa aliyethibitishwa na mkaguzi wa afya mahali pa kazi, kuwa hatakiwi kufanya kazi katika eneo analokumbwa na madini ya risasi anarejea kazini, hadi mkaguzi wa afya mahali pa kazi athibitishe kwa maandishi kwamba mfanyakazi anaweza kufanya kazi hiyo.

(4) Mwajiri atahakikisha kuwa-

(a) mfanyakazi wa kike ambaye ana uwezo wa kuzaa na anafanya kazi inayomuweka katika kukumbwa na madini ya risasi, anaondolewa kwenye kazi hiyo wakati mkusanyiko wake wa damu unazidi $40\mu g/100\ m\ell$ au kiwango cha madini ya risasi kwenye mkojo unazidi $75\mu g/\ell$, au endapo ana ujauzito; na

(b) mfanyakazi anayetajwa katika kanuni ndogo ya (4)(a) haruhusiwi kurejea katika kazi ambayo itamweka katika kukumbwa na madini ya risasi, isipokuwa kama kiwango

chake cha madini ya risasi katika damu ni chini ya 30µg/100 mℓ au kiwango cha madini ya risasi kwenye mkojo ni chini ya 65µg/ℓ, au endapo kuondolewa kulitokana na ujauzito, mfanyakazi hana ujauzito tena.

Ukanda wa kuvaa kifaa kinga cha kupumulia

8. Mwajiri au mtu aliyejiajiri atahakikisha kwamba-

(a) mahali pa kazi au sehemu ya mahali pa kazi ambapo kiwango cha madini ya risasi katika hewa kipo au kinaweza kuwa kikubwa zaidi ya kikomo cha kukumbwa na madini hayo endapo mtu hajavaa kifaa kinga cha kupumulia, itengwe kama ukanda wa kuvaa kifaa kinga cha kupumulia;
(b) eneo lililotengwa la ukanda wa kuvaa vifaa kinga vya kupumulia linawekwa ishara za usalama zinazoonesha kwamba eneo husika ni ukanda wa kuvaa kifaa kinga cha kupumulia kama ilivyoainishwa katika kanuni ya 12;
(c) hakuna mtu anaingia au kufanya kazi katika ukanda wa kuvaa vifaa kinga vya kupumulia bila kuwa amevaa vifaa kinga husika; na
(d) sababu ya kuongezeka kwa kiwango cha madini ya risasi katika hewa inatambuliwa na hatua za haraka zinachukuliwa mbali na kuvaa vifaa kinga vya kupumulia ili kupunguza kiwango cha madini ya risasi chini ya kikomo.

Kumbukumbu

9. Mwajiri atatakiwa -

(a) kuweka kumbukumbu za matokeo ya tathmini zote, ufuatiliaji wa hewa, taarifa za uchunguzi wa afya na maboresho ya hatua za udhibiti zinazohitajika na kanuni za 6, 7 na 8 kwa muda usiopungua miaka thelathini:

    Isipokuwa kwamba, kumbukumbu binafsi za matibabu atapatiwa mkaguzi wa afya tu au endapo mfanyakazi ataruhusu kwa maandishi apatiwe mtu mwingine;
(b) kumpatia mkaguzi taarifa za tathmini zote na

ufuatiliaji wa hewa ili kubaini kiwango cha kukumbwa na madini ya risasi;

(c) kutunza kumbukumbu zote za ufuatiliaji wa afya kwa muda usiopungua miaka thelathini na ikiwa mwajiri atasitisha shughuli anazofanya, akabidhi au awasilishe kumbukumbu zote kwa Mkaguzi Mkuu, kwa kuzingatia kwamba kumbukumbu hizo zitakuwa angalau na-

(i) jina la ukoo la mfanyakazi, majina ya awali, jinsia, tarehe ya kuzaliwa, jina la mwenzi wa ndoa au ndugu wa karibu zaidi na anwani ya kudumu;

(ii) kumbukumbu ya aina ya kazi iliyofanywa ambayo ilisababisha mfanyakazi kukumbwa na madini ya risasi, eneo ambalo wafanyakazi wamekumbwa, tarehe ya kuanza na kumaliza kazi husika, na muda wa kukumbwa na madini ya risasi katika masaa kwa wiki;

(iii) kumbukumbu ya kukumbwa na madini ya risasi inayohusiana na kazi ya awali kabla ya ajira ya sasa ya mfanyakazi; na

(iv) tarehe za ufuatiliaji wa afya na matokeo yake.

(d) kutunza kumbukumbu za mafunzo ya kinadharia na vitendo aliyopewa mfanyakazi kwa mujibu wa kanuni ya 4 kwa muda wote mfanyakazi atakapokuwa kwenye ajira.

Udhibiti wa kukumbwa na madini ya risasi

10.-(1) Mwajiri au mtu aliyejiajiri atahakikisha kwamba kukumbwa na madini ya risasi katika mahali pa kazi kunazuiwa au kudhibitiwa vya kutosha, udhibiti huo utachukuliwa kuwa wa kutosha endapo-

(a) kiwango cha madini ya risasi katika hewa kipo chini ya kikomo cha kukumbwa na madini ya risasi kazini, au kama kipo juu ya kikomo, sababu imetambuliwa na hatua ya haraka

tofauti na kugawa vifaa kinga vya kupumulia imechukuliwa ili kupunguza kiwango hicho; na

(b) ikiwa kuna hali ya kukumbwa na-

(i) madini ya risasi yanayoweza kumezwa, kiwango cha madini ya risasi ni chini ya 20µg/100 mℓ kwenye damu; au

(ii) madini ya risasi ya tetra-alkyl, kiwango cha madini ya risasi ni chini ya 120µg/ℓ kwenye mkojo.

(2) Mwajiri au mtu aliyejiajiri atadhibiti uwezekano wa mtu kukumbwa na madini ya risasi kwa -

(a) kutumia mbadala wa madini ya risasi au bidhaa zenye mchanganyiko wa madini ya risasi;

(b) kupunguza au kudhibiti idadi ya watu wanaoweza kukumbwa na madini ya risasi;

(c) kupunguza muda ambao mtu atakumbwa au anaweza kukumbwa na madini ya risasi;

(d) kupunguza kiwango cha madini ya risasi ambacho kinaweza kuingia katika mazingira ya kazi;

(e) kuanzisha hatua za udhibiti wa kihandisi ili kupunguza kukumbwa na madini ya risasi kama-

(i) kutenganisha mchakato wa uzalishaji, kutumia mitambo peke yake au kufungia;

(ii) ufungaji wa mifumo ya kutoa hewa chafu karibu na chanzo ili kudhibiti uzalishaji wa madini ya risasi katika hewa;

(iii) kumwagia maji ili kupunguza vumbi lenye madini ya risasi;

(iv) kutenganisha maeneo ya kazi yenye uzalishaji tofauti; na

(v) utambuzi wa hatua za haraka za urekebishaji zinazopaswa kuchukuliwa.

(f) kuanzisha taratibu salama za maandishi za

ufanyaji kazi ambazo mfanyakazi lazima azingatie ili kuhakikisha kuwa -

(i) madini ya risasi yanatumika na yanaondolewa mahali pa kazi kwa usalama;

(ii) mitambo ya uzalishaji, vifaa, zana, uchimbaji, na mifumo ya kutoa hewa chafu katika chanzo inatumiwa kwa usalama na kutunzwa; na

(iii) hatua sahihi za awali za kurekebisha udhibiti wa kukumbwa na madini ya risasi zinachukuliwa.

Vifaa kinga

11.-(1) Mwajiri au mtu aliyejiajiri atatakiwa -

(a) Kuwapatia wafanyakazi na watu ambao wanaweza kukumbwa na madini ya risasi katika hewa katika kiwango kinachozidi nusu ya kikomo cha kukumbwa na madini ya risasi kazini, mavazi ya kazi ambayo hayana mifuko ili kupunguza uwezekano wa kubeba vumbi lenye madini ya risasi;

(b) kuhusiana na madini ya risasi ya tetra-alkyl ambayo yanaweza kufyonzwa kupitia ngozi, kumpa mtu vifaa kinga ambavyo havipitishi madini ya risasi kwenye ngozi; na

(c) kumpa vifaa kinga vya kupumulia ili kuhakikisha kuwa kukumbwa na madini ya risasi katika hewa kunadhibitiwa.

(2) Pale ambapo kifaa kinga cha kupumulia kimetolewa, mwajiri au mtu aliyejiajiri atahakikisha kwamba -

(a) kifaa husika kinauwezo wa kuweka kiwango cha kukumbwa na madini ya risasi chini ya kikomo cha kukumbwa kazini kulingana na aina ya madini ya risasi;

(b) kifaa kinga sahihi kimechaguliwa kwa usahihi na kutumika ipasavyo;

(c) taarifa, maelekezo, mafunzo na usimamizi wa matumizi ya vifaa kinga inafahamika kwa watu; na

(d) vifaa vinawekwa katika hali nzuri na utaratibu mzuri wa kufanya kazi.

(3) Mwajiri au mtu aliyejiajiri atahakikisha -

(a) kutowapatia watu vifaa kinga ambavyo tayari vimetumika, isipokuwa kama vifaa hivyo vimesafishwa na kutakaswa kwa namna ambayo haitaruhusu madini ya risasi kuingia katika mazingira ya kazi; na

(b) kuwa sehemu ya kuhifadhia vifaa kinga wakati ambapo havitumiki.

Usafi wa majengo na mitambo

12. Kila mwajiri au mtu aliyejiajiri atahakikisha-

(a) sehemu zote za kazi zinawekwa katika hali ya usafi bila taka zenye madini ya risasi, na pale ambapo madini ya risasi yanapomwagika au kupeperushwa na upepo mahali pa kazi, hatua za kurekebisha zichukuliwe mara moja, kabla ya kazi yoyote kuendelea;

(b) usafi unafanyika na kifaa kinachoweza kuvuta uchafu chenye ufanisi wa kuchuja angalau asilimia 99 ya chembe zenye ukubwa wa maikromita moja, ili vumbi lenye madini ya risasi lisiingie hewani kuchafua mahali pa kazi au mazingira;

(c) vifaa vya kuvuta uchafu vinakarabatiwa na kusafishwa kwa wakati ili kuondoa vumbi la madini ya risasi; na

(d) pale ambapo matumizi ya vifaa vya kuvuta uchafu haiwezekani, sehemu zinazopaswa kusafishwa zinawekwa maji na watu wanaofanya usafi huo wanavaa mavazi sahihi na vifaa kinga vya kupumulia.

Kudumisha hatua za udhibiti

13. Mwajiri au mtu aliyejiajiri atahakikisha kwamba-

(a) vifaa vyote vya udhibiti vinatunzwa katika hali na mpangilio mzuri wa kufanya kazi; na

(b) hatua za udhibiti wa kihandisi zipimwe na zijaribiwe kila baada ya miezi kumi na mbili au itakavyoelekezwa na mkaguzi.

Kuweka lebo, ufungaji, usafiri na uhifadhi

14. Mwajiri au mtu aliyejiajiri, ili kuzuia usambaaji wa madini ya risasi atahakikisha kwamba-

(a) madini ya risasi yaliyohifadhiwa au kusambazwa yanatambulika ipasavyo, yanainishwa na kutumika kwa mujibu wa taratibu za afya na usalama; na

(b) kontena au gari ambalo madini ya risasi yanasafirishwa, limebainishwa bayana na kupakiwa kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali.

Sura ya 177

Mazuio

15.-(1) Mwajiri au mtu aliyejiajiri hataruhusu mtu yeyote kufanya kazi katika mazingira ambayo kiwango cha madini ya risasi kitazidi kiwango cha kikomo cha kukumbwa.

(2) Mtu yeyote hataruhusiwa -

(a) kutumia hewa iliyo katika mgandamizo kupuliza chembe chembe za madini ya risasi kutoka kwenye sehemu yoyote;

(b) kuvuta sigara, kula, kunywa au kuweka chakula au vinywaji ndani ya eneo ambalo halijatengwa mahususi kwa ajili hiyo; na

(c) kupaka rangi yenye madini ya risasi ndani ya majengo au samani, kufuta au kusugua rangi yenye madini ya risasi katika sehemu kavu au kuondoa rangi yenye madini ya risasi kwa kuchoma.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 7(2)(b) na (c))*

SEHEMU A
VIPINDI VYA KUCHUKUA VIPIMO VYA KIWANGO CHA MADINI YA RISASI KWENYE DAMU

| Damu yenye madini ya risasi µg/100 mℓ | Ukomo wa Vipindi vya Kuchukua Vipimo vya Madini ya Risasi Kwenye Damu |
|---|---|
| chini ya 20 | miezi 12 |
| 20 - 39 | miezi 6 |
| 40 - 59 | miezi 3 |
| 60 na zaidi | Kwa maelekezo ya mkaguzi wa afya mahali pa kazi. |

SEHEMU B
VIPINDI VYA KUCHUKUA VIPIMO VYA KIWANGO CHA MADINI YA RISASI KWENYE MKOJO

| Mkojo Wenye Madini ya Risasi µg/ℓita | Ukomo wa Vipindi vya Kuchukua Vipimo vya Madini ya Risasi Kwenye Mkojo |
|---|---|
| chini ya 120 | wiki 6 |
| 120 - 149 | wiki 1 |
| 150 na zaidi | Kwa maelekezo ya mkaguzi wa afya mahali pa kazi. |

Dodoma,
3rd April, 2023

JOYCE L. NDALICHAKO,
*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mku,*
*(Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu)*

TANGAZO LA SERIKALI Na. 288 la tarehe 7/4/2023

SHERIA YA AFYA NA USALAMA MAHALI PA KAZI,
(SURA YA 297)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 109)*

KANUNI ZA EGONOMIA ZA MWAKA 2023

## MPANGILIO WA KANUNI

*Kanuni* *Jina*

1. Jina.
2. Tafsiri.
3. Matumizi.
4. Taarifa na mafunzo.
5. Wajibu wa wanaoweza kukumbwa na visababishi vya hatari za egonomia.
6. Wajibu wa wasanifu, watengenezaji na wasambazaji.
7. Tathmini ya hatari za egonomia.
8. Udhibiti wa hatari.
9. Ufuatiliaji wa afya.
10. Utunzaji wa vidhibiti.
11. Utunzaji wa kumbukumbu.

)

SHERIA YA AFYA NA USALAMA MAHALI PA KAZI,
(SURA YA 297)

---

## KANUNI

---

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 109)*

KANUNI ZA EGONOMIA ZA MWAKA 2023

Jina

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Egonomia za Mwaka 2023.

Tafsiri

2. Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo -

"egonomia utambuzi" maana yake ni kuboresha uhusiano kati ya vipengele vya utambuzi na utendaji.

"majeraha na matatizo ya misuli na mifupa" maana yake ni madhara ya mwili ambayo yanaathiri misuli, viungo, mishipa na mishipa ya fahamu kwa kusababisha maumivu, kufa ganzi, uvimbe au kupoteza utendaji kazi wake.

"mbunifu" maana yake ni -

(a) mtu aliyebobea ambaye-
   (i) anakagua na kupitisha kazi iliyosanifiwa;
   (ii) anampangia mtu aliye chini yake ikiwemo mfanyakazi kutayarisha sanifu; au
   (iii)kubuni kazi zinazofanyika kwa muda mfupi, ikiwa ni pamoja na vitu vinavyohusika.

(b) msanifu majengo au mhandisi anayechangia au kuwa na jukumu la jumla la kufanya sanifu;

(c) mhandisi wa miundombinu ya jengo anayeandaa michoro ya kiufundi inayoainisha namna ya ufungaji na upachikaji wa mitambo

isiyohamishika; au

(d) mkadiriaji majenzi anayebainisha viwango vya vitu vinavyotakiwa.

"mfumo wa misuli na mifupa" maana yake ni mfumo wa mifupa, misuli na tishu unganishi ambao hulinda mwili wa binadamu na viungo vyake, na ndio msingi wa viungo kusogea na kufanya kazi;

" mbobezi kuhusiana na egonomia" maana yake ni mtu ambaye-

(a) kuhusiana na kazi inayotakiwa kufanywa, ana ujuzi, mafunzo na uzoefu unaohitajika katika nyanja ya egonomia; na

(b) anaifahamu sheria na kanuni zinazotumika zilizoundwa chini ya Sheria.

"programu ya egonomia" maana yake ni utaratibu wa kutarajia, kutambua, kuchambua na kudhibiti visababishi hatari vya egonomia ya mwili na utambuzi, ambayo itajumuisha angalau utambuzi wa vihatarishi vya egonomia na tathmini ya hatari, udhibiti wa hatari, ufuatiliaji wa tathmini ya taarifa na mafunzo na ufuatiliaji wa afya;

Sura ya 297

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Afya na Usalama Mahali Pa Kazi;

"tathmini ya hatari ya egonomia" maana yake ni mpango unaofanywa ili kubaini hatari yoyote ya kukumbana na vihatarishi vya egonomia mahali pa kazi ili kutambua hatua zinazohitajika kuchukuliwa, kuondoa, kupunguza au kudhibiti hatari hiyo;

"utambuzi" maana yake ni utafsiri wa vichocheo kutoka kwenye mazingira na ndani ya mwili wa mtu ambapo Vichocheo hivi hupitishwa na viungo vya hisia mpaka kwenye ubongo; na

"visababishi vya hatari vya egonomia" maana yake ni vitendo vinavyofanyika mahali pa kazi, mazingira ya kazi, au mchanganyiko, ambavyo vinaweza kusababisha au kuzidisha matatizo ya misuli na mifupa yanayohusiana na kazi.

Matumizi

3. Kanuni hizi zitatumika kwa-

(a) mwajiri au mtu aliyejiajiri ambaye anafanya kazi mahali ambapo panaweza kumuweka mtu yeyote kwenye visababishi hatari vya egonomia za mwili au egonomia utambuzi; na

(b) watu wanaosanifu, wanaotengeneza, wanaosimika au kusambaza mashine au vifaa vya kutumika kazini.

Taarifa na mafunzo

4.-(1) Mwajiri, baada ya kushauriana na Kamati ya Afya na Usalama iliyoundwa mahali pa kazi chini ya usimamizi wake au wawakilishi wa afya na usalama walioteuliwa kwenye sehemu hiyo ya kazi au vitengo tofauti tofauti vya kazi, ataweka kwa ajili ya wafanyakazi wote, au watu wengine mbali na wafanyakazi, ambao wanaweza kuathiriwa na hatari za egonomia, mpango wa mafunzo unaojumuisha-

(a) maudhui na wigo wa matumizi ya Kanuni hizi;

(b) vyanzo vya kukumbana na visababishi vya hatari za egonomia;

(c) asili ya visababishi vya hatari za egonomia;

(d) hatari ya afya inayohusiana na visababishi vya hatari za egonomia;

(e) kiwango ambacho wanaweza kuwa katika hatari;

(f) vidhibiti hatari vilivyopo katika eneo la kazi;

(g) utoaji taarifa mapema za kutojisikia vizuri au dalili zinazohusiana kwa mwakilishi wa afya na usalama au mwajiri;

(h) tahadhari za kuchukuliwa na mfanyakazi kujilinda dhidi ya hatari za kiafya zinazohusiana visababishi vya hatari za egonomia;

(i) tathmini ya kukumbwa na vihatarishi vya egonomia, madhumuni ya ufuatiliaji, ulazima wa ufuatiliaji wa afya na faida za muda mrefu za ufuatiliaji wa afya; na

(j) utaratibu wa kutoa taarifa za kasoro katika mitambo au vifaa ambavyo vinaweza

kusababisha majeraha ya misuli na mifupa.

(2) Mafunzo yanayokusudiwa katika kanuni ndogo ya (1) yataendeshwa kwa wafanyakazi wote waliopo kazini.

(3) Mafunzo ya kukumbushana yatafanywa kila mwaka au kwa vipindi ambavyo vinaweza kupendekezwa na Kamati ya Afya na Usalama au wawakilishi wa afya na usalama au mkaguzi.

(4) Mafunzo yanayokusudiwa katika kanuni ndogo ya (1) yatatolewa na mtu ambaye ni mbobezi wa masuala ya afya na usalama mahali pa kazi na ameidhinishwa na Mkaguzi Mkuu.

(5) Mwajiri au mtu aliyejiajiri atahakikisha kadiri inavyowezekana kwamba, wafanyakazi wake au watu wengine ambao siyo wafanyakazi wake ambao wanaweza kuathiriwa na visababishi vya hatari za egonomia mahali pa kazi wanapewa taarifa, maelekezo na mafunzo ya kutosha.

(6) Mwajiri atatunza kumbukumbu za mafunzo yoyote ambayo mfanyakazi amepewa kwa mujibu wa kanuni hii.

Wajibu wa wanaoweza kukumbwa na visababishi hatari za egonomia

5. Mtu yeyote ambaye anakumbwa au anayeweza kukumbwa na visababishi vya hatari za egonomia atatii maelekezo yoyote halali aliyopewa na mwajiri au mtu aliyejiajiri au na mtu yeyote aliyeidhinishwa na mwajiri au mtu aliyejiajiri, kuhusu -

(a) utekelezaji wa hatua zilizopitishwa kudhibiti visababishi vya hatari za egonomia;
(b) kushirikiana na mwajiri katika kazi ya kutambua namna mfanyakazi anaweza kukumbwa na visababishi vya hatari za egonomia;
(c) kutoa taarifa mapema za kutojisikia vizuri au dalili zinazohusiana kwa mwakilishi wa afya na usalama au mwajiri;
(d) kutoa taarifa mara moja ya kasoro katika mitambo au vifaa vinavyoweza kusababisha majeraha na matatizo ya misuli na mifupa kwa mwakilishi wa afya na usalama au

mwajiri;

(e) taarifa na mafunzo yaliyotolewa kama ilivyoainishwa katika kanuni ndogo ya 4.

Wajibu wa wasanifu, watengenezaji na wasambazaji

6.-(1) Wasanifu wa mitambo, mashine, vifaa au vitu vya kutumika kazini watalazimika -

(a) kuondoa visababishi vya hatari za egonomia kwenye usanifu wa kifaa au endapo haiwezekani, kupunguza visababishi vya hatari za egonomia ambavyo wafanyakazi wanaweza kukumbwa navyo katika kutumia au mwingiliano na kifaa hicho wakati wa utendaji wa kazi;

(b) kutoa taarifa kuhusu visababishi vya hatari za egonomia zilizotambuliwa na udhibiti kwa mtengenezaji ili aweze kuchukua hatua wakati wa utengenezaji, na vyovyote vile inavyowezekana, kuondoa au kupunguza visababishi vya hatari za egonomia vilivyobakia wakati wa usanifu na kuhakikisha kuwa hakuna hatari mpya inayoletwa wakati wa mchakato wa utengenezaji; na

(c) kutoa taarifa kwa mtengenezaji au msambazaji, kama msanifu anatengeneza bidhaa kwa ajili ya watumiaji husika kuhusu visababishi vya hatari za egonomia ambavyo hajaweza kuondoa wakati wa usanifu na masharti yanayohitajika kwa matumizi salama.

(2) Watengenezaji wa mitambo, mashine, vifaa au vitu vya kutumika kazini watatakiwa-

(a) kutengeneza vitu au jengo au miundo mbinu ambayo ni salama;

(b) kutumia nyenzo ambazo hupunguza visababishi vya hatari za egonomia kuanzia wakati wa ujenzi, na wakati bidhaa zinatumiwa, na wakati wa kazi za mikono;

(c) kutumia na kupima hatua za usalama zilizoainishwa na msanifu katika utengenezaji; na

(d) kutoa taarifa kwa msambazaji, kwa watumiaji wanaohusika katika matumizi ya bidhaa kuhusu matumizi salama ya bidhaa na hatari ambazo hazijaondolewa katika hatua ya usanifu.

(3) Mtu yeyote anayesambaza au kuuza mitambo, mashine, vifaa au vitu kwa ajili ya matumizi ya kazini atatakiwa-

(a) kusambaza au kuuza bidhaa ambazo ni salama;

(b) kuuza bidhaa zinazoweza kusafirishwa, kupokelewa, kutunzwa na kushughulikiwa kwa usalama;

(c) kutoa maelezo na mafunzo kwa watumiaji watarajiwa wanaohusika katika kila matumizi yaliyotambuliwa ya bidhaa kuhusu masharti yanayohitajika kwa matumizi salama na visababishi vya hatari za egonomia ambayo havijaondolewa au kupunguzwa kadri inavyowezekana katika hatua za ubunifu, utengenezaji au uuzaji;

(d) kusimika vifaa au kujenga jengo kwa kutumia nyenzo salama na, kwa namna, na katika maeneo ambayo itahakikishwa kuwa nyenzo zinaendeshwa kwa usalama; na

(e) kuwasiliana na mtumiaji kuhusu matengenezo yanayohitajika ili kuhakikisha matumizi na uendeshaji.

Tathmini ya hatari za egonomia

7.-(1) Mwajiri atatakiwa-

(a) kabla ya kuanza kwa kazi yoyote ambayo inaweza kuwaweka wafanyakazi katika visababishi vya hatari za egonomia, kuwepo tathmini ya hatari za egonomia inayofanywa na kuidhinishwa na Mamlaka; na

(b) kuweka matokeo ya tathmini ya hatari za egonomia kwenye kumbukumbu kama

ilivyoainishwa katika kanuni ya 11.

(2) Tathmini ya hatari inayotajwa katika kanuni ndogo ya (1) itajumuisha-

(a) utambuzi wa vihatarishi vya egonomia na visababishi vya hatari za egonomia ambavyo watu wanaweza kukumbana navyo;

(b) uchambuzi na tathmini ya visababishi vya hatari za egonomia na vihatarishi vilivyotambuliwa kupitia nyaraka mbalimbali;

(c) mpango na utaratibu salama wa kazi unaotumika ili kupunguza au kudhibiti visababishi vya hatari za egonomia na vihatarishi ambavyo vimetambuliwa;

(d) ufuatiliaji wa mpango kazi; na

(e) mapitio ya mipango.

(3) Mwajiri atahakikisha kwamba wafanyakazi wote walio chini ya usimamizi wake wanafahamishwa, wanaelekezwa na kufundishwa na mtaalamu kuhusu vihatarishi vyovyote na taratibu zinazohusiana na kazi na; au hatua za kudhibiti kabla ya kazi kuanza; na baada ya kazi kuanza kulingana na mpango wa ufuatiliaji wa tathmini ya hatari na mapitio.

(4) Mwajiri atapitia tathmini ya hatari za egonomia iliyofanywa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1) endapo-

(a) kuna sababu ya kuamini kwamba tathmini hiyo haikidhi mahitaji;

(b) hatua za udhibiti hazina ufanisi;

(c) maendeleo ya kiteknolojia au kisayansi yanaruhusu mbinu bora zaidi za udhibiti;

(d) kama mabadiliko yanaathiriwa kwa namna ambayo kazi inayofanywa inaweza kuleta mabadiliko ya visababishi vya hatari ya egonomia; au

(e) kama kuna tukio limetokea.

Udhibiti wa hatari

8.-(1) Mwajiri au mtu aliyejiajiri atahakikisha kwamba mtu kukumbwa na visababishi vya hatari za egonomia vinazuiwa au, ikiwa haiwezekani,

vinadhibitiwa ipasavyo.

(2) Kwa madhumuni ya kutekeleza kanuni ndogo ya (1), mwajiri au mtu aliyejiajiri atatakiwa, kwa kadri inavyowezekana, kuondoa au kupunguza uwezekano wa kukumbwa na visababishi vya hatari za egonomia kwa kutekeleza hatua za udhibiti katika mpangilio ufuatao wa kipaumbele-

(a) hatua za udhibiti wa kihandisi ili kuondoa au kupunguza visababishi vya hatari; na
(b) hatua za udhibiti za kiutawala kupunguza idadi ya watu na muda wa kukumbwa na hatari.

Ufuatiliaji wa afya

9.-(1) Mwajiri atahakikisha kuwa mfanyakazi anafanyiwa ufuatiliaji wa afya endapo -

(a) matokeo ya tathmini yanaonesha kwamba mfanyakazi amekumbwa na visababishi vya hatari za egonomia kwa kiasi kikubwa;
(b) kuathiriwa kwa wafanyakazi na visababishi vya hatari za egonomia ni kama vile-
(i) ugonjwa unatambulika au athari mbaya ya kiafya inaweza kuhusishwa na kukumbana na visababishi vya hatari za egonomia;
(ii) kuna uwezekano wa kutosha kwamba ugonjwa au athari za kiafya zinaweza kutokea katika hali fulani mahali pa kazi na kuna mbinu za kugundua dalili za ugonjwa au athari za kiafya kadiri inavyowezekana; au
(iii) mtaalamu wa afya ya mazingira ya kazi amependekeza kwamba wafanyakazi husika wanapaswa kuwa chini ya ufuatiliaji wa afya katika hali ambayo mwajiri anaweza kumwita mtaalamu wa afya wa magonjwa yanayotokana na kazi kuridhia usahihi wa mapendekezo hayo.

(2) Mwajiri atahakikisha kwamba ufuatiliaji wa afya unaokusudiwa katika kanuni ndogo ya (1)

unajumuisha-

(a) tathmini ya awali ya afya kwa wafanyakazi wapya kabla ya kuanza ajira au ndani ya siku kumi na nne baada ya mtu kuanza ajira ya kazi hatarishi, au kwa wafanyakazi wengine wote katika ajira, ndani ya miezi ishirini na nne ya tarehe ya kuanza kwa kanuni hii, hii inajumuisha -

(i) tathmini ya historia ya afya na kazi aliyokuwa anafanya;

(ii) uchunguzi wa mwili; na

(iii) uchunguzi mwingine wowote muhimu ambao kwa maoni ya daktari wa magojwa yatokanayo na kazi ni muhimu kuwezesha tathimini ipasavyo;

(b) tathmini ya mara kwa mara ya afya;

(c) dodoso za kutambua dalili kwa wafanyakazi walio katika kazi hatarishi, katika vipindi visivyozidi miaka miwili, au kwa vipindi vilivyoainishwa na daktari wa magonjwa yanayotokana na kazi; Isipokuwa kwamba ikiwa dalili zimeonekana, tathmini zaidi inapaswa kufanywa kama inavyokusudiwa katika Kanuni ndogo ya 2 (a) (ii) na (iii); na

(d) uchunguzi wa misuli na mifupa baada ya ajira kukoma.

(3) Mwajiri hatamruhusu mfanyakazi ambaye amethibitishwa kuwa hafai kufanya kazi na daktari wa magonjwa yanayotokana na kazi, kufanya kazi mahali pa kazi ambapo anaweza kukumbwa na vihatarishi vya egonomia, isipokuwa mfanyakazi husika anaweza kuruhusiwa kurudi katika kazi ambayo anaweza kukumbwa na vihatarishi vya egonomia iwapo atathibitishwa kuwa imara kuweza kufanya kazi hiyo na daktari wa magonjwa yanayotokana na kazi.

(4) Mwajiri atachunguza na kuweka kumbukumbu za matukio yote ambayo yanapelekea mfanyakazi kupata matatizo ya misuli na mifupa yanayohusiana na kazi.

Utunzaji wa vidhibiti

10. Mwajiri au mtu aliyejiajiri atahakikisha kwamba kitu chochote anachotoa kwa manufaa ya wafanyakazi katika kutekeleza majukumu yake chini ya kanuni hizi -

(a) kinatumika kikamilifu na ipasavyo; na

(b) kinatunzwa katika hali ya ufanisi na katika utaratibu mzuri wa kufanya kazi.

Utunzaji wa kumbukumbu

11. Mwajiri au mtu aliyejiajiri atatakiwa -

(a) kutunza kumbukumbu za matokeo ya taarifa zote za tathmini na ufuatiliaji wa afya na utunzaji wa vidhibiti unaohitajika na kanuni hizi;

(b) kwa kuzingatia masharti Kanuni ndogo 1(c), kuweka kumbukumbu za taarifa za afya zinazokusudiwa katika Kanuni ndogo 1 (a) apatiwe mkaguzi wakati wa ukaguzi;

(c) kwa kuzingatia kibali rasmi cha maandishi cha mfanyakazi, kuruhusu mtu yeyote kusoma taarifa za afya kuhusiana na mfanyakazi husika;

(d) kuweka kumbukumbu za tathmini zote zipatikane kwa ajili ya kusomwa na mwakilishi husika wa afya na usalama au kamati husika ya afya na usalama;

(e) kutunza kumbukumbu zote za tathmini kwa muda usiopungua miaka thelathini;

(f) kutunza kumbukumbu zote za ufuatiliaji wa afya kwa muda usiopungua miaka thelathini, na ikiwa mwajiri atasitisha shughuli anazofanya, akabidhi au awasilishe kumbukumbu zote kwa Mkaguzi Mkuu; kwa kuzingatia kwamba kumbukumbu hizo zitakuwa na angalau taarifa zifuatazo:

(i) jina la ukoo la mfanyakazi, majina ya awali, jinsia, tarehe ya kuzaliwa, jina la mwenzi wa ndoa au ndugu wa karibu zaidi na anwani ya kudumu;

(ii) kumbukumbu ya aina ya kazi

iliyofanywa ambayo ilisababisha mfanyakazi kukumbwa na visababishi vya hatari za egonomia, eneo ambalo wafanyakazi wamekumbwa na vihatarishi, tarehe ya kuanza na kumaliza kazi husika, na muda wa kukumbwa na hatari katika masaa kwa wiki;

(iii) kumbukumbu ya kukumbwa na visababishi vya hatari za egonomia vinavyohusiana na kazi ya awali kabla ya ajira ya sasa ya mfanyakazi; na

(iv) tarehe za ufuatiliaji wa afya na matokeo yake. kuweka kumbukumbu ya mafunzo aliyopewa mfanyakazi kwa muda wote ambao yupo kwenye ajira ambapo anakumbwa na visababishi vya hatari za egonomia.

Dodoma,
………………, 2023

JOYCE L. NDALICHAKO,
*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu*
*(Kazi, Vijana, Ajira, na*
*Wenye Ulemavu)*

TANGAZO LA SERIKALI Na. 289 la tarehe 7/4/2023

SHERIA YA AFYA NA USALAMA MAHALI PA KAZI,
(SURA YA 297)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 109)*

KANUNI ZA MAZINGIRA YA KAZI ZA MWAKA 2023

## MPANGILIO WA KANUNI

*Kanuni* *Jina*

1. Jina.
2. Tafsiri.
3. Matumizi.
4. Mahitaji ya hali joto.
5. Mwanga.
6. Utofautishaji wa uoni.
7. Hewa na uingizaji hewa
8. Mpangilio wa mazingira ya kazi.
9. Kelele na kuhifadhi usikivu.
10. Udhibiti wa vumbi.
11. Kuondoa au kudhibiti kukumbwa na mitetemo.
12. Kinga dhidi ya kukumbwa na mionzi ayonishi.

SHERIA YA AFYA NA USALAMA MAHALI PA KAZI,
(SURA YA 297)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 109)*

KANUNI ZA MAZINGIRA YA KAZI ZA MWAKA 2023

Jina

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Mazingira ya Kazi za Mwaka 2023.

Tafsiri

2. Katika Kanuni hizi isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo -

"balaklava" maana yake ni vazi linalofunika kichwa na shingo isipokuwa sehemu ya uso;

"Kielezo cha Halijoto ya Balbu Mnyevu (WBGT)" maana yake ni namba inayobainisha kiwango cha hali ya joto katika mazingira ya kazi;

"kifaa kinga cha upumuaji" maana yake ni kifaa ambacho huvaliwa kufunika angalau mdomo na pua ili kuzuia kuvuta hewa ambayo si salama;

"kiharusi cha joto" maana yake ni hali ya kiafya inayotokana na kushindwa kwa mwili wa binadamu kudhibiti joto;

"kipimo cha sauti (dBA)" maana yake ni kipimo cha kiwango cha sauti hewani kama inavyotambuliwa na masikio ya binadamu;

"kikomo cha dozi mahali pa kazi" kiwango cha juu cha kukumbwa na mionzi ayonishi kinachoruhusiwa ambacho kinapimwa katika mSv/mwaka au mrem/mwaka;

"kishikizi cha taa" maana yake ni kifaa kinachoshikilia taa na kuiunganisha na umeme;

"kukumbwa na vihatarishi kila siku" maana yake ni hali ya mfanyakazi kukumbwa na vihatarishi kuanzia masaa nane ya kazi kwa siku na kuendelea;

"kiwango cha kikomo cha ukumbwaji" maana yake ni kiwango cha ukumbwaji wa kila siku kilichowekwa katika kanuni za kazi ambacho hakipaswi kuzidi;

"kiwango cha ukumbwaji cha kuchukua hatua" maana yake ni kiwango cha ukumbwaji wa kila siku kilichowekwa katika kanuni za kazi yoyote ambacho kikifikiwa au kikizidi inahitaji hatua maalum ili kupunguza hatari;

"kiwango sawa cha shinikizo la sauti" maana yake ni kiwango sawa cha sauti inayoendelea kutoa kiasi sawa cha nguvu ya sauti kama sauti halisi inayobadilika badilika, inayopimwa kwa muda sawa;

"kuzoea" maana yake ni kuzoea hali ya mabadiliko ya viambata vya mazingira ambavyo mfanyakazi anakumbana navyo;

"mitetemo ya kiganja-mkono" maana yake ni mitetemo inayosababishwa na mashine ambayo hupitishwa kwenye kiganja na mikono wakati wa kazi;

"mtetemo wa mwili mzima" maana yake ni mtetemo unaosababishwa na mashine ambao hupitishwa ndani ya mwili mzima wa mfanyakazi akiwa amekaa au kusimama wakati wa kufanya kazi;

"mwanga" maana yake ni kiwango cha mwangaza kinachofika katika eneo la kazi, ambacho husomwa kwa kizio cha lux;

"mwangaza elekezwa" maana yake ni mwangaza ambao mionzi ya mwanga huwekwa kwenye mwalo mwembamba uliobainishwa vyema;

"sehemu kwa milioni/trilioni (ppm/ppt)" maana yake ni kizio cha ujazo wa kiambata cha hewa ya mahali husika;

Sura ya 297 "Sheria" maana yake ni Sheria ya Afya na Usalama Mahali Pa Kazi;

"shughuli za ujenzi" maana yake ni ujenzi, urekebishaji wa miundo, ukarabati au matengenezo ya jengo, inajumuisha kupaka rangi, kupamba upya na usafi wa nje wa jengo, ubomoaji wa jengo na maandalizi ya uwekaji wa msingi wa jengo lililokusudiwa, lakini haijumuishi operesheni yoyote ambayo ni kazi za majenzi ya kihandisi;

"ukanda wa kelele" maana yake ni eneo ambalo kiwango cha

kelele ni sawa au kinazidi kiwango cha katazo;

"uwanda wa kufanyia kazi" maana yake ni eneo la mlalo ambapo kazi inafanywa;

"uwezo wa kupunguza" maana yake ni uwezo uliothibitishwa wa vilinda usikivu ili kupunguza kiwango cha kelele ambacho mvaaji anakumbana nacho;

"vilinda usikivu" maana yake ni mofu za masikio au vizibo vya masikio vya viwango vinavyotambulika; na

"wastani wa kipimo kwa nyakati tofauti" maana yake ni wastani wa idadi ya vipimo wakilishi ambavyo huchukuliwa kwa kipindi cha muda fulani.

Matumizi

3. Kanuni hizi zitatumika mahali pa kazi na kwa mtu aliyejiajiri ambaye anatakiwa kumlinda mtu yoyote anayefika katika eneo lake la kazi.

Mahitaji ya hali joto

4.-(1) Kwa mujibu wa masharti ya kanuni ndogo ya (2), mwajiri hatamruhusu mfanyakazi kufanya kazi katika mazingira ambayo wastani wa hali joto ya balbu kavu iliyopimwa kwa kipindi cha muda wa masaa manne ni chini ya nyuzi joto 6, isipokuwa mwajiri atachukua hatua zinazofaa kumlinda mfanyakazi huyo dhidi ya baridi na kuchukua tahadhari zote muhimu kwa usalama wa mfanyakazi huyo, isipokuwa pale ambapo kazi ya nje inafanywa, mwajiri atachukua hatua hizo na tahadhari kama hizo katika mazingira ambayo halijoto ya balbu kavu ni chini ya nyuzi joto 6 wakati wote.

(2) Mwajiri hatamruhusu mfanyakazi kufanya kazi katika mazingira ya jokofu ambapo kipimo cha hali joto ya balbu kavu iko chini ya nyuzi joto 0 isipokuwa -

(a) muda wa juu wa mfanyakazi kukumbwa na hali joto hauzidi muda ulioainisha katika Jedwali la Nne la Kanuni hizi.

(b) mfanyakazi amepewa mavazi ya kinga yafuatayo-

(i) suti ya nailoni ya kujikinga na baridi kali, ambapo halijoto iliyopimwa iko chini ya nyuzi joto hasi thelathini na nne, vazi hilo litakuwa la safu mbili;

(ii) balaklava ya sufi;

(iii) glavu za ngozi zenye manyoya;

(iv) glavu zisizopitisha maji zenye sufi iliyosokotwa kwa ndani na aproni isiyopitisha maji ambapo vitu vyenye unyevu au kuyeyushwa hushughulikiwa;

(v) soksi za sufi; na

(vi) buti zisizopitisha maji,

Isipokuwa kwamba, mfanyakazi anayefanya kazi katika eneo lenye halijoto ya chini ambayo halijoto yake si chini ya nyuzi joto hasi kumi na nane kwa muda usiozidi dakika tano katika kila saa anahitaji tu kupewa viatu vinavyofunika mguu.

(c) mfanyakazi kabla ya kuanza kufanya kazi, na baada ya hapo kila mwaka awe amethibitishwa anaweza kufanya kazi katika mazingira hayo kwa mujibu wa kifungu cha 24 cha Sheria; na

(d) nguo zote zinazovaliwa na mfanyakazi zinatakiwa ziwe kavu kabla ya kuingia katika eneo la joto la chini.

(3) Mwajiri atatakiwa kufuatilia uingiaji kwenye vyumba vya baridi ili kuhakikisha wafanyakazi hawakai muda mrefu ili kupunguza madhara na mfumo wa udhibiti wa uingiaji unafuatwa.

(4) Pale ambapo zana zinazoshikiliwa kwa mkono ambazo hutetema kwa kasi ya mtetemo wa chini ya 1000 Hz hutumika kwenye halijoto halisi ya balbu kavu chini ya nyuzi joto sita, mwajiri atampa mfanyakazi anayeendesha zana hizo glavu mahususi kwa kazi hiyo.

(5) Endapo wastani wa kielezo cha halijoto ya balbu mnyevu (WBGT), iliyopimwa kwa muda wa saa moja inazidi thelathini (WBGT) katika mazingira ambayo mfanyakazi anafanya kazi, mwajiri huyo atatakiwa -

(a) kuchukua hatua za kupunguza kielezo cha halijoto hadi chini ya 30 cha balbu mnyevu (WBGT); au

(b) ikiwa imeshindikana kupunguza hadi chini ya thelathini ya kielezo cha balbu mnyevu (WBGT) na pale ambapo kazi ngumu ya mikono inafanywa -

(i) kila mfanyakazi kabla ya kuanza kufanya

kazi, na baada ya hapo kila mwaka awe amethibitishwa anaweza kufanya kazi katika mazingira hayo na daktari aliyeidhinishwa, iwapo atathibitika kuwa ana uwezo wa kufanya kazi katika mazingira hayo, apewe cheti cha uthibitisho;

(ii) kuhakikisha kwamba kila mfanyakazi huyo amezoea mazingira hayo ya kazi kabla ya kuhitajika au kuruhusiwa kufanya kazi katika mazingira hayo;

(iii) kumuelimisha kila mfanyakazi uhitaji wa kunywa angalau mililita mia sita za maji kila saa;

(iv) utoa mafunzo kwa kila mfanyakazi juu ya tahadhari zinazopaswa kuchukuliwa ili kuepuka kiharusi cha joto; na

(v) isipokuwa pale ambapo kuna walakini wa kuwepo kazi ngumu za mikono, mapendekezo ya mkaguzi yataamua.

Mwanga

5.-(1) Kila mwajiri atahakikisha katika sehemu yake ya kazi kuna mwanga kulingana na viwango vya mwangaza kama vilivyoainishwa kwenye Jedwali la Kwanza, isipokuwa pale ambapo mwanga maalum ni muhimu kwa ajili ya utendaji wa aina fulani ya kazi, bila kujali kama aina hiyo ya kazi imeorodheshwa kwenye Jedwali au la, mwajiri atahakikisha wafanyakazi wanaofanya kazi hiyo wanakuwa kwenye mazingira yenye mwanga unaohitajika.

(2) Kuhusiana na mwanga uliotajwa katika kanuni ndogo ya (1), waajiri watahakikisha kwamba-

(a) wastani wa mwanga ndani ya mita tano kutoka sehemu ambapo mfanyakazi anafanya kazi usiwe chini ya moja ya tano ya wastani wa mwanga unaohitajika kwa kazi hiyo;

(b) uakisi mwanga katika sehemu yoyote ya kazi umepunguzwa hadi kiwango ambacho hakiathiri uwezo wa kuona;

(c) mwanga kwenye mashine zinazozunguka zenye hatari ya athari za mwanga unaowaka na

kuzimika ziondolewe; na

(d) vishikizi vya taa na taa viwekwe safi na, vinapokuwa na kasoro, vibadilishwe au kurekebishwa mara moja.

(3) Kwa hali ya dharura inayohitaji kuondoka haraka eneo la kazi la ndani ambalo halina mwanga asilia au ambalo watu wanafanya kazi kwa kawaida usiku, kila mwajiri atatakiwa, katika sehemu hizo za kazi, kutoa vyanzo vya dharura vya mwanga ambavyo pale vinapowashwa, vinatoa mwanga usiopungua lux1, ili kuwezesha wafanyakazi kuondoka kwa haraka mahali pa kazi,

Isipokuwa kwamba, pale ambapo ni lazima kusimamisha mashine au kuzima mitambo au michakato kabla ya kuondoka kwa haraka mahali pa kazi, au ambapo vifaa hatari vipo au michakato hatari inafanywa, mwanga hautatakiwa kuwa chini ya lux 20.

(4) Mwajiri atahakikisha kwamba vyanzo vya dharura vya mwanga vilivyoainishwa katika kanuni ndogo ya (3)-

(a) zina uwezo wa kujiwashwa ndani ya sekunde 15 baada ya kushindwa kwa mwanga ulioainishwa na kanuni ndogo ya (1);

(b) itadumu kwa muda wa kutosha ili kuhakikisha kuondoka kwa haraka mahali pa kazi kwa usalama;

(c) zimewekwa katika mpangilio mzuri wa kufanya kazi na zinajaribiwa ufanisi wake katika kila kipindi kisochozidi miezi mitatu; na

(d) pale ambapo vishikizi mwelekeo vya taa vimewekwa, viwekwe kwenye urefu usiopungua mita mbili juu ya usawa wa sakafu na visielekezwe juu ya nyuzi kumi na chini ya nyuzi arobaini na tano ya mstari wa usawa ambao vishikizi hivyo vimewekwa.

(5) Mwajiri anayejishughulisha na shughuli za ujenzi katika eneo lake la kazi atahakikisha vyumba vyote, ngazi, njia za kupita, vyumba vya chini ya ardhi na sehemu nyinginezo ambazo hatari inaweza kuwepo kwa kukosa mwanga wa asili, kuweka mwanga ili kuwe salama.

Utofautishaji wa uoni

6.-(1) Ili kutofautisha uoni wa mahali pa kazi na maeneo ya nje ya mahali pa kazi ambapo wafanyakazi wanafanya kazi sehemu kubwa ya zamu zao katika chumba ambacho eneo la sakafu ni chini ya mita za mraba mia moja, mwajiri atahakikisha kila chumba kinawekwa madirisha kwa njia ambayo -

(a) ukubwa wa madirisha hayo usiwe chini ya theluthi tatu ya kipeuo cha pili cha eneo la sakafu ya chumba, na maeneo yote mawili yawe yamepimwa kwa mita za mraba;

(b) ukomo wa dirisha hauko juu na vichwa vya dirisha haviko chini ya mita moja na nusu juu ya usawa wa sakafu ya chumba; na

(c) madirisha hayo yawekewe uzio unaopitisha mwanga.

(2) Isipokuwa, kama mkaguzi ataagiza vinginevyo, masharti ya kanuni ndogo ya (1) hayatatumika kwenye mazingira ambapo mwanga wa asili utakuwa na athari mbaya kwa mchakato wa kazi au nyenzo zinazotumika katika chumba, au pale ambapo mchakato katika chumba unapaswa kufanywa chini ya mazingira yaliyodhibitiwa ya hali ya mwanga, joto, unyevu au mzunguko wa hewa, au ambapo uamuzi wa muundo au rangi katika chumba unahitaji mazingira yenye kiwango cha mwanga chenye ubora, au kwa sababu za kiusalama, faragha au ulinzi, kufuata masharti yaliyokusudiwa inakuwa haiwezekani.

(3) Endapo kupenya kwa mwanga wa jua moja kwa moja katika sehemu yoyote ya kazi kunaweza kuleta tishio kwa usalama wa wafanyakazi katika sehemu hiyo ya kazi, mwajiri atahakikisha kuwa anaweka kizuizi katika sehemu hiyo ya kazi ili kuepuka kupenya huko, lakini afanye hivyo bila kuathiri mahitaji ya uoni katika chumba hicho.

Hewa na uingizaji hewa

7.-(1) Mwajiri atahakikisha kwamba kila sehemu ya mahali pa kazi inapitisha hewa kwa njia ya asili au ya kimakenika kwa namna ambayo-

(a) hewa inayovutwa na wafanyakazi haihatarishi usalama na afya zao;

(b) kiwango cha wastani cha ujazo wa kaboni dayoksaidi kilichopo katika hewa, na kilichopimwa kwa muda wa masaa nane, au muda

mwingine wowote wa kazi hakizidi 1000 ppm;

(c) kiwango cha ukomo wa kukumbwa na viambata vya kwenye hewa hakizidi kama ilivyoainishwa katika Sehemu ya A ya Jedwali la Tano la Kanuni hizi;

(d) kiwango kilichopo cha gesi inayoweza kulipuka au kuwaka hakizidi kiwango cha chini cha kulipuka kama ilivyoainishwa katika Sehemu A ya Jedwali la Tano la Kanuni hizi; na

(e) maeneo ya kazi yenye ufinyu wa hewa ya asili yatakuwa na ufuatiliaji endelevu wa gesi wakati wote wa kazi.

(2) Pale ambapo hatua zilizowekwa chini ya kanuni ndogo ya (1) hazitekelezeki, au kuna hatari ya hewa isiyo salama katika usawa wa kupumulia wa mfanyakazi, mwajiri atampa kila mfanyakazi husika na kuhakikisha kwamba anatumia kwa usahihi vifaa kinga vya kupumulia vya aina ambayo hupunguza kukumbwa na vihatarishi vya kwenye hewa kwa kiwango salama, na mwajiri atamfahamisha mfanyakazi juu ya vihatarishi vilivyopo na hatua za tahadhari dhidi ya kukumbwa kupita kiasi na vihatarishi hivyo.

Mpangilio wa mazingira ya kazi

8.-(1) Mtumiaji wa mashine atatoa na kuweka nafasi ya kutosha ya wazi na isiyozuiliwa katika kila mashine ili kuwezesha kazi kufanyika bila kuhatarisha usalama wa wafanyakazi.

(2) Mwajiri atatakiwa -

(a) bila kujumuisha sehemu za kazi ambazo shughuli za ujenzi zinafanyika, aweke angalau mita za mraba 2.25 za eneo la sakafu lililo wazi kwa kila mfanyakazi anayefanya kazi katika eneo la kazi la ndani;

(b) kuwepo na nafasi isiyo na kizuizi katika eneo la kazi kwa kila
mfanyakazi;

(c) kuweka kila sehemu ya kazi ya ndani katika hali ya usafi, mpangilio mzuri, na kuondoa vifaa, zana na vitu ambavyo havihitajiki kwa kazi inayofanywa katika sehemu hiyo ya kazi;

(d) kuweka sakafu, njia, na ngazi zote katika hali ya usalama, kusiwepo vizuizi, utelezi, taka na zana; na

(e) kuweka paa na kuta za kila sehemu ya kazi ya ndani katika ubora bila kuvuja.

(3) Mwajiri hatamruhusu mtu yeyote kutupa kitu chochote kutoka mahali pa juu isipokuwa kwa kutumia kinyanyuzi, au kama kuna utaratibu umewekwa wa kuhakikisha usalama unakuwepo kwa vitu vinavyoanguka.

Kelele na kuhifadhi usikivu

9.-(1) Kanuni hii itatumika mahali pa kazi ambapo mfanyakazi katika sehemu hiyo ya kazi anakumbwa na kiwango sawa cha kelele cha 85 dB(A) au zaidi.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (3) na (4), mwajiri hatamruhusu mfanyakazi kufanya kazi katika mazingira ambayo anakumbwa na kiwango sawa cha kelele cha 85 dB(A) au zaidi.

(3) Mwajiri atapunguza kiwango sawa cha kelele hadi chini ya 85 dB(A) au, ikiwa hii haiwezekani, atapunguza kiwango hicho kadri inavyowezekana na kuchukua hatua zote zinazofaa kuzuia kelele kutoka kwenye chanzo.

(4) Ikiwa kiwango sawa cha kelele katika sehemu yoyote ya kazi hakiwezi kupunguzwa hadi chini ya 85 dB(A), kama ilivyokusudiwa katika kanuni ndogo ya (3), mwajiri atatakiwa -

(a) kuweka ishara inayoashiria kelele kwenye ukanda wenye kelele katika eneo hilo la kazi na katika milango ya kuingia na kutoka kwenye chumba ambacho kina kelele; na

(b) kumkataza mtu yeyote kuingia katika eneo la kelele isipokuwa kama mtu huyo amevaa vilinda usikivu.

(5) Katika shughuli za ujenzi ambapo haiwezekani kufuata masharti ya kanuni ndogo ya (4)(a) kutokana na asili au ukubwa wa eneo, mwajiri ataweka ishara hizo katika eneo la kuingia na kutoka, au ataweka ishara kama hizo mahali pa wazi karibu iwezekanavyo na mahali pa kazi husika au mahali ambapo mkaguzi anaweza kuelekeza.

(6) Pale ambapo kwa maoni ya mkaguzi, mwajiri

ameacha au ameshindwa kupunguza kiwango sawa cha kelele katika eneo la kelele hadi chini ya 85 dB(A) au kutenga chanzo cha kelele anaweza kumuamuru mwajiri huyo kwa notisi ya maandishi, kuchukua hatua zaidi kwa kadri ambayo mkaguzi ataona kuwa ni za busara na zinazotekelezeka kwa madhumuni ya kuhifadhi usikivu wa wafanyakazi wanaoingia au kufanya kazi katika eneo hilo la kelele.

(7) Mwajiri atatakiwa atoe bila malipo, vilinda usikivu kwa kila mfanyakazi anayefanya kazi ndani au, kwa mtu yeyote anayehitajika au kuruhusiwa kuingia eneo la kelele, na mwajiri hataruhusu mtu yeyote kufanya kazi au kuingia eneo la kelele isipokuwa kama amevaa vilinda usikivu kwa njia sahihi.

(8) Vilinda usikivu ambavyo mwajiri atatoa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (7) vitakuwa -

(a) vimeridhiwa na mkaguzi kwamba, mwajiri amechukua hatua za kutosha za tahadhari ili kuhakikisha kwamba matumizi ya kawaida ya vilinda usikivu hayatasababisha kuenea kwa magonjwa ya kuambukiza, na ameidhinisha matumizi ya kawaida ya vilinda usikivu hivyo;

(b) vinatunzwa na mwajiri katika hali bora na ya usafi wakati wote; na

(c) vinahifadhiwa kwenye chombo safi kisicho na vumbi kilichotolewa

na mwajiri wakati havitumiki.

(9) Mwajiri atatakiwa kutoa maelezo kwa mtu yeyote anayetakiwa kuvaa vilinda usikivu matumizi ya vilinda usikivu hivyo, na kumtaarifu kuhusu ukanda wenye kelele ambapo uvaaji ni walazima.

(10) Mwajiri atatakiwa -

(a) kuhakikisha kuwa kila mfanyakazi aliyeajiriwa katika ukanda wenye kelele anafanyiwa uchunguzi wa usikivu unaofanywa kwa mujibu wa kifungu cha 24 cha Sheria, na mkaguzi wa afya aliyeidhinishwa na Mkaguzi Mkuu;

(b) kutunza kumbukumbu za uchunguzi wa usikivu na kuhakikisha anapatiwa mkaguzi iwapo atazihitaji; na

(c) kutunza kumbukumbu hizo kwa muda usiopungua miaka thelathini baada ya kukoma kwa ajira, isipokuwa pale ambapo mwajiri atasitisha kazi, atoe taarifa kwa Mkaguzi Mkuu.

(11) Katika kutekeleza masharti ya kanuni ndogo ya (4)(a), mwajiri atapokea maelekezo kutoka Mamlaka ya ukaguzi iliyoidhinishwa.

(12) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni hii, wastani wa viwango vya kelele vinavyoruhusiwa mahali pa kazi, ni kama vilivyoainishwa katika Jedwali la Pili la Kanuni hizi.

Udhibiti wa vumbi

10.-(1) Mwajiri atahakikisha kwamba kikomo cha vumbi hakizidi kiwango kilichoainishwa katika Jedwali la Tano.

(2) Mwajiri atahakikisha kazi zozote zinazofanyika katika mahali pa kazi, zana au bidhaa anazotumia hazizalishi vumbi, au apunguze uzalishaji wa vumbi.

(3) Pale ambapo mwajiri atashindwa kutekeleza masharti ya kanuni ndogo ya (2) atatakiwa kufanya yafuatayo-

(a) ufuatiliaji wa kiwango cha vumbi kinachozalishwa katika eneo lake la kazi na kiwango cha vumbi ambacho mfanyakazi husika anakumbwa; na

(b) anaweka miundo mbinu ya za kuweza kudhibiti vumbi katika mahali pa kazi ili kiwango cha kukumbwa na vumbi kiwe chini ya kikomo kwa kufanya yafuatayo-

kuweka kizuizi kati ya mfanyakazi na chanzo cha vumbi, au kutenga kazi zinazozalisha vumbi na kazi zingine katika mahali pa kazi;

(i) kuweka kifaa karibu na chanzo cha vumbi au miundo mbinu inayovuta na kutoa vumbi nje ya eneo la kazi;

(ii) kufanya usafi wa mara kwa mara wa mitambo, mashine, nyaraka, vifaa, samani, paa za nyumba, madirisha, sakafu, kuta, maeneo yaliyojificha na yasiyotumika kwa namna ambayo haisababishi vumbi kusambaa,

(iii) kusafisha maeneo ya kazi kwa kutumia kifaa cha kuvuta uchafu badala ya fagio kwa maeneo ambayo italazimika kufanya hivyo ili kuondoa vumbi; na

(iv) kumwagia maji eneo lenye vumbi ili kuondoa vumbi linalosambaa hewani;

(4) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (3), mwajiri atapunguza muda wa kukumbwa kwa wafanyakazi katika maeneo yenye vumbi, au kubadilisha wafanyakazi wanaofanya katika maeneo yenye vumbi au kufanya kazi zinazozalisha vumbi katika sehemu ya kazi ili kupunguza athari za kukumbwa na vumbi kwa wafanyakazi husika.

(5) Mwajiri atawapatia wafanyakazi wanaofanya kazi katika maeneo yenye vumbi, au wanaofanya kazi zinazozalisha vumbi au watu wowote wanaofika katika maeneo yenye vumbi katika sehemu ya kazi vifaa kinga vya kupumulia sahihi, kwa kuzingatia kiwango cha vumbi, muda wa kukumbwa, na aina ya vumbi linalozalishwa katika eneo la kazi kama itavyoelekezwa na mkaguzi.

(6) Mwajiri au mtu aliyejiajiri lazima atoe taarifa, maelekezo na mafunzo kwa watu kuhusu-

(a) chanzo cha kukumbwa na vumbi;

(b) athari za kiafya na usalama zinazoambatana na kukumbwa kwa vumbi;

(c) tahadhari muhimu za kuchukua ili kupunguza kukumbwa na vumbi;

(d) matumizi sahihi ya vifaa kinga vya kupumulia; na

(e) njia salama za kufanya kazi ili kuzuia au kupunguza uzalishaji wa vumbi.

(7) Mwajiri atahakikisha-

(a) kila mfanyakazi aliyeajiriwa katika maeneo yenye vumbi au anafanya kazi zinazozalisha vumbi anafanyiwa uchunguzi wa mapafu unaofanywa kwa mujibu wa Sheria, na mkaguzi wa afya aliyeidhinishwa na Mkaguzi Mkuu;

(b) anatunza kumbukumbu za uchunguzi wa mapafu na kuhakikisha anapatiwa mkaguzi iwapo atazihitaji; na

(c) anatunza kumbukumbu hizo kwa muda usiopungua miaka thelathini baada ya kukoma

kwa ajira, isipokuwa pale ambapo mwajiri atasitisha kazi, atoe taarifa kwa Mkaguzi Mkuu.

Kuondoa au kudhibiti kukumbwa na mitetemo

11.(1) Mwajiri au mtu aliyejiajiri atahakikisha kuwa-

(a) katika sehemu yake ya kazi anatumia mitambo, mashine, vifaa au zana ambazo hazizalishi mitetemo; au

(b) anatumia mitambo, mashine, vifaa na zana ambazo zinazalisha mitetemo katika kiwango salama.

(2) Pale ambapo haiwezekani kutekeleza masharti ya kanuni ndogo ya (1), mwajiri atapunguza muda wa mfanyakazi kukumbwa na mitetemo kwa-

(a) kupunguza muda wa mfanyakazi kukumbwa na mitetemo ya mwili au mkono; na

(b) kufanya kazi kwa awamu kwa wafanyakazi wanaokumbwa na mitetemo ya mwili na mkono.

(3) Ili kuzuia mitetemo ya mwili mzima mwajiri atatakiwa-

(a) kuweka kikomo cha muda unaotumiwa na wafanyakazi kwenye sehemu au mtambo yenye mitetemo kama ilivyoainishwa katika Sehemu A ya Jedwali la Sita la Kanuni hizi;

(b) kuhakikisha kuwa kifaa au mashine inatunzwa, kuboreshwa au kurekebishwa pale inapohitajika ili kupunguza mitetemo; na

(c) anaweka kifaa kinachosaidia kupunguza mitetemo katika viti;

(4) Ili kuzuia mitetemo ya kwenye mikono, mwajiri atatoa glavu maalum za kuzuia mitetemo, pamoja na kufanya yafuatayo-

(a) kutoa zana zenye vishikio vinavyohitaji nguvu ndogo ya mikono ambayo bado itaruhusu utumiaji salama wa zana na mchakato husika,

(b) kusimamia uvaaji wa glavu ili kuzuia mitetemo

(c) kutoa vipindi vya kupumzika katika muda wa kazi ili kupunguza muda wa wafanyakazi kukumbwa na mitetemo

(d) kuweka ukomo wa muda wa kuvumilia mtetemo

wa mkono kama ilivyoainishwa katika Sehemu B ya Jedwali la Sita ya Kanuni hizi;

(e) kukataza matumizi ya zana zenye kasoro; na

(f) kuboresha, kurekebisha, au kubadilisha zana ambazo zimechakaa, butu au zisizo na mpangilio.

(5) Mwajiri atafanya ufuatiliaji wa mitetemo kwa wafanyakazi, kwa kutumia vifaa husika vya kupima mitetemo ya mikono na mwili kwa wafanyakazi wote wanaotumia zana, vifaa au kuendesha mashine zinazozalisha mitetemo.

(6) Mwajiri atatoa mafunzo kwa wafanyakazi ya namna sahihi ya kutumia zana na vifaa vinavyotetema na kuzitunza ili kupunguza kukumbwa na mitetemo kwa kiwango kikubwa.

(7) Mwajiri atahakikisha-

(a) kila mfanyakazi anayefanya kazi katika maeneo, mashine, mitambo au anatumia zana na vifaa vyenye mitetemo anafanyiwa uchunguzi wa afya, unaofanywa kwa mujibu wa Sheria, na mkaguzi wa afya aliyeidhinishwa na Mkaguzi Mkuu;

(b) anatunza kumbukumbu za uchunguzi wa afya na kuhakikisha anapatiwa mkaguzi iwapo atazihitaji; na

(c) anatunza kumbukumbu hizo kwa muda usiopungua miaka thelathini baada ya kukoma kwa ajira, isipokuwa pale ambapo mwajiri atasitisha kazi, lazima atoe taarifa kwa Mkaguzi Mkuu.

Kinga dhidi ya kukumbwa na mionzi ayonishi

12.-(1) Mwajiri anayetumia vifaa vya mionzi au chanzo cha mionzi ayonishi au kushiriki katika shughuli zinazohusisha kukumbwa na mionzi ayonishi atahakikisha kwamba-

(a) wafanyakazi wanakingwa dhidi ya kukumbwa na mionzi ayonishi;

(b) mtu yeyote asikumbwe na mionzi ayonishi inayozidi kiwango kilichoainishwa katika Jedwali la Tatu;

(c) mfanyakazi au mtu yeyote anayeingia katika maeneo yenye mionzi ya kuchaji anapatiwa kifaa

stahiki au beji inayovaliwa ili kufuatilia kikomo cha kuathiriwa na mionzi;

(d) anatoa vifaa kinga stahiki na vya kutosha ili kulinda usalama na afya za wafanyakazi;

(e) kunakuwepo na wakufunzi wenye sifa kwa ajili ya kutoa mafunzo ya mara kwa mara yanayohusiana na mionzi ayonishi, mafunzo yatolewe kwa kuzingatia majadiliano kati ya mwajiri na wafanyakazi au wawakilishi wa usalama na afya mahali pa kazi.

(2) Mfanyakazi wa kike anayefanya kazi katika maeneo yenye mionzi ayonishi baada ya kufahamu kuwa ni mjamzito atamjulisha mwajiri ili mazingira yake ya kazi yaweze kuboreshwa, mwajiri ataboresha mazingira ya kazi kwa kuzingatia kiwango cha madhara husika, ili kuhakikisha kuwa mtoto aliyeko tumboni pia anapewa kiwango sawa cha ulinzi kama ilivyoanishwa katika Jedwali la Tatu.

(3) Mfanyakazi hataruhusiwa na kukumbwa zaidi ya kiwango cha juu cha kipimo cha mionzi ayonishi kwa mwaka mmoja kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Tatu, isipokuwa-

(a) kwa madhumuni ya kuokoa maisha au kuzuia majeraha makubwa;

(b) ikiwa anachukua hatua zinazolenga kuzuia kiwango kikubwa cha mionzi;

(c) ikiwa anachukua hatua za kudhibiti hali ya janga kuendelea.

(4) Chombo kinachohifadhi kiambata chenye mionzi ambacho hakijafungwa kitawekwa alama za kudumu zifuatazo:

(a) jina au alama ya mtengenezaji;

(b) alama ya kemikali, kiwango cha kemikali inayozalisha mionzi, na ikiwezekana jina la maandalizi ya kemikali; na

(c) kiwe na neno "RADIOACTIVE".

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 5(1))*

Wastani wa Viwango vya Mwanga Vinavyotakiwa Katika Eneo la Kazi
(Imepimwa Kwenye Eneo la Kazi)

| Eneo la kazi | Kiwango cha chini (lux) | Kiwango cha juu (lux) |
|---|---|---|
| Ofisi | 200 | 750 |
| Varanda | 100 | 750 |
| Stoo | 100 | 750 |
| Jikoni | 100 | 750 |
| Kiwandani | 100 | 750 |
| Kazi Za ufinyanzi | 100 | 750 |
| Vyooni | 100 | 750 |

| Eneo la kazi | Kiwango cha chini (lux) | Kiwango cha juu (lux) |
|---|---|---|
| Maabara | 200 | 750 |
| Chumba cha mkutano | 200 | 750 |
| Ukumbi wa mikutano | 150 | 750 |
| Kazi za kuchora | 500 | 750 |
| Chumba cha kusanifu | 200 | 750 |
| Kazi inayohitaji umakini mkubwa | 500 | 1000 |
| Uchimbaji wa Chini ya ardhi | 100 | 300 |

## JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 9(12))*

Wastani wa Viwango vya Kelele Vinavyoruhusiwa Katika Eneo la Kazi

| Leq dB (A) | Muda (Kila siku) | Muda (Kila Wiki) |
|---|---|---|
| 85 | saa 8.00 | saa 40.00 |
| 88 | saa 4.00 | saa 20.00 |
| 91 | saa 2.00 | saa 10.00 |
| 94 | saa 1.00 | saa 5.00 |
| 97 | dakika 30.00 | saa 2.50 |
| 100 | dakika 15.00 | saa 1.25 |
| 103 | dakika 7.50 | dakika 37.5 |
| 106 | dakika 3.75 | dakika 18.75 |
| 109 | dakika 1.87 | dakika 9.37 |

## JEDWALI LA TATU

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 12(1)(b))*

Ukomo wa Kukumbwa na Mionzi ayonishi Katika Eneo la Kazi

| Eneo Katika Mwili | Kikomo cha dozi ya Kukumbwa | |
|---|---|---|
| | mrem/mwaka | mSv/mwaka |
| mwili mzima | 5000 | 50 |
| sehemu ya mwili | 50000 | 500 |
| ngozi | 50000 | 500 |
| kwenye lenzi ya jicho | 15000 | 150 |
| mtoto aliyeko tumboni | 500 | 5 |

## JEDWALI LA NNE

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 4(2)(a))*

KIWANGO CHA SHINIKIZO LA JOTO

| Aina ya Mavazi | WBGT (°C) |
|---|---|
| Mavazi ya Kazi (Shati la mikono mirefu na Suruali) | 0 |
| Vazi yaliyotengenezwa kwa malighafi iliyosokotwa | 0 |
| Ovaroli ya plastic | + 0.5 |
| Ovaroli ya plastic isiyopitisha maji | + 1 |
| Mavazi ya tabaka mbili | + 3 |
| Ovaroli ya kuzuia mvuke | + 11 |

Kukumbwa na Shinikizo la Joto (WBGT katika °C) kwa masaa 8 ya kazi kwa siku juma moja

| Mpangilio wa Kazi | Kuzoea | | | | Kiwango cha kuchua hatua (kutokuzoea) | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kazi Nyepesi | Kazi ya Kawaida | Kazi Nzito | Kangi nzito Sana | Kazi Nyepesi | Kazi ya Kawaida | Kazi Nnzito | Kangi nzito Sana |
| 75-100% | 31.0 | 28.0 | -- | -- | 28.0 | 25.0 | -- | -- |
| 50-75% | 31.0 | 29.0 | 27.5 | -- | 28.5 | 26.0 | 24.0 | -- |
| 25-50% | 32.0 | 30.0 | 29.0 | 28.0 | 29.5 | 27.0 | 25.5 | 24.5 |
| 0-25% | 32.5 | 31.5 | 30.5 | 30.0 | 30.0 | 29.0 | 28.0 | 27.0 |

Mifano ya uzito wa kazi:

kupumzika - kukaa, kwa harakati za wastani za mkono

kazi nyepesi - kukaa au kusimama ili kudhibiti mashine, kufanya kazi nyepesi ya mkono au kiganja kwa mfano kutumia msumeno wa meza,kutembea mara kwa mara, kuendesha gari

kazi ya wastani - kutembea na kuinua kwa wastani na kusukuma au kuvuta; kutembea kwa kasi ya wastani, kusugua sehemu kwa kusimama

kazi nzito - kazi ya kuchukua na koleo, kuchimba, kubeba, kusukuma / kuvuta mizigo mizito kutembea kwa kasi, k.m. seremala akishona kwa mkono

nzito sana - shughuli kali sana kwa kasi ya juu, k.m. kusukuma mchanga wenye unyevu

JEDWALI LA TANO

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 7(1)(c)(d) na 10(1))*

VIWANGO VINAVYOKUBALIKA VYA UKOMO WA VIAMBATA VYA HEWA NA VUMBI

*Tangazo la Serikali Na.289 (Linaendelea.)*

SEHEMU A

Kiwango cha Ubora wa Hewa

| Viambata vya Hewa | Kiwango cha Ukomo wa Kukumbwa | Muda (masaa) |
|---|---|---|
| Kaboni monoksaidi | 35ppm | 8 |
| Kiwango cha chini cha mlipuko | kisizidi 5% | Muda wowote |
| Kaboni dayoksaidi | kisizidi 1000ppm ikiwa ndani ya jengo<br>kisizidi 4000 ppm ikiwa nje | Muda wowote |
| naitrojeni dayoksaidi | 40ppm | 8 |
| salfa dayoksaidi | kisizidi 1ppm | 8 |
| Unyevu wa kwenye hewa ndani ya jengo | kiwe kati ya 30% na 70% | Muda wowote |
| Mzuguko wa hewa | kisipungue 0.5m/s na kisizidi 2m/s | Muda wowote |
| ozoni | kisizidi 78ppm | 8 |
| formaldehyde | kisizidi 0.5ppm | 8 |
| oksijeni | Kisipungue 19% na kisizidi 23% | |

| Chembe chembe kuanzia 2.5µm (PM2.5) | | | |
|---|---|---|---|
| Aina ya Chembe chembe | Kipimo katika µm | | Ukomo katika ppm |
| | ukomo wa chini | ukomo wa juu | kiasi cha kuvumilika |
| silica | 2.5 | 5.0 | 0.05 |
| vumbi la mbao ngumu | 2.5 | 5.0 | 1.0 |
| vumbi la mkaa | 2.5 | 5.0 | 3.0 |
| vumbi la mbao laini | 2.5 | 5.0 | 5.0 |
| vumbi la pamba | 2.5 | 5.0 | 1.0 |
| vumbi la katani | 2.5 | 5.0 | 1.0 |
| vumbi la muwa | 2.5 | 5.0 | 1.0 |
| vumbi lolote | 2.5 | 5.0 | 5.0 |

SEHEMU B

Kiwango cha Ukomo wa Vumbi

JEDWALI LA SITA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni 11(3)(a))*

UKOMO WA KUVUMILIA MTETEMO WA MWILI MZIMA

| Ukomo wa kukumbwa kila siku | Kiwango cha juu cha kukumbwa kila siku | Kiwango cha kuchukua hatua ya kukumbwa |
|---|---|---|
| saa 8 | 1.15 $m/s^2$ | 0.5 $m/s^2$ |

UKOMO WA KUVUMILIA MTETEMO WA MKONO

| Ukomo wa kukumbwa kila siku | Kiwango cha juu cha kukumbwa kila siku | Kiwango cha kuchukua hatua ya kukumbwa |
|---|---|---|
| saa 8 | 5 $m/s^2$ | 2.5 $m/s^2$ |

Dodoma,
………………, 2023

JOYCE L. NDALICHAKO,
*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu*
*(Kazi, Vijana, Ajira, na*
*Wenye Ulemavu)*

TANGAZO LA SERIKALI Na. 290 la tarehe 7/4/2023

SHERIA YA AFYA NA USALAMA MAHALA PA KAZI,
(SURA YA 297)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 109)*

KANUNI ZA UFANYAJI KAZI BILA KUTUMIA ZANA ZA MWAKA 2023

MPANGILIO WA KANUNI

*Kanuni* *Jina*

1. Jina.
2. Tafsiri.
3. Matumizi.
4. Wajibu wa mtu zaidi ya mmoja.
5. Utambuzi na tathmini ya hatari za kazi zinazohusisha ufanyaji kazi bila kutumia zana.
6. Wajibu wa wasanifu, watengenezaji, waagizaji na wasambazaji.
7. Tathmini ya hatari.
8. Wajibu wa mwajiri kwa mkandarasi anayejitegemea na Majukumu mengine yanayohusiana.
9. Mwajiri kushauriana na mwakilishi wa Afya na usalama.
10. Wajibu wa mwajiri wa kutambua kazi hatarishi zinazohusisha ufanyaji kazi bila kutumia zana.
11. Wajibu wa mwajiri kufanya tathmini ya hatari.
12. Wajibu wa mwajiri kudhibiti hatari.
13. Wajibu wa mfanyakazi.

SHERIA YA AFYA NA USALAMA MAHALA PA KAZI,
(SURA YA 297)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 109)*

KANUNI ZA UFANYAJI KAZI BILA KUTUMIA ZANA ZA MWAKA 2023

Jina

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Ufanyaji Kazi Bila Kutumia Zana za Mwaka 2023.

Tafsiri

2. Katika Kanuni hizi isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"hatari"maana yake ni uwezekano wa kupata jeraha, maumivu au ugonjwa kutokana na kukumbwa na kihatarishi;

"kihatarishi" maana yake ni uwezekano wa kusababisha jeraha, maumivu au ugonjwa;

"kitu" inajumuisha kitu kisicho hai au chenye uhai, mtambo na kitu chochote au viambata vilivyomo ndani ya kitu;

"matatizo ya misuli na mifupa" maana yake ni jeraha, maumivu au ugonjwa unaotokea kwa ujumla au kwa sehemu kutokana na ufanyaji kazi bila kutumia zana mahali pa kazi, uwe unatokea ghafla au kwa muda mrefu, lakini haijumuishi jeraha, maumivu au ugonjwa unaosababishwa na kupondwa, kunaswa au kukatwa kunakotokana na uendeshaji wa mitambo;

"matumizi ya nguvu kubwa" kuhusiana na ufanyaji kazi bila kutumia zana, maana yake ni matumizi ya nguvu ambayo ingetarajiwa kwamba watu wengi mahali pa kazi, au watu wanaoweza kufanya kazi hiyo, watakuwa na ugumu katika kuitekeleza na inajumuisha nguvu inayohitajika kunyanyua vitu vizito, kusukuma au kuvuta vitu ambavyo ni

vigumu kusogeza, kuendesha zana zilizoundwa kwa mkono mmoja ikiwa ni lazima kwa mikono miwili kutumika, na kutumia zana zinazohitaji kubana kwa vishikizo vilivyo na umbali kati yao;

Sura ya 297

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Afya na Usalama Mahali Pa Kazi; na

"ufanyaji kazi bila kutumia zana" maana yake ni kazi yoyote anayoifanya mfanyakazi inayohitaji matumizi ya nguvu kuinua, kusukuma, kuvuta, kubeba, kusogeza, kushikilia au kuzuia kitu chochote.

Matumizi

3. Kanuni hizi zitatumika katika maeneo yote ya kazi ambayo yanahusisha ufanyaji kazi bila kutumia zana.

Wajibu wa mtu zaidi ya mmoja

4. Pale ambapo, kwa mujibu wa Kanuni hizi, wajibu umewekwa kwa mtu zaidi ya mmoja, wajibu huo lazima ufanywe na kila mtu kwa masuala ambayo mtu huyo ana usimamizi au udhibiti nayo na kama mtu mwingine yeyote anawajibika au la kwa ajili ya kutekeleza wajibu huo.

Utambuzi na tathmini ya hatari za kazi zinazohusisha ufanyaji kazi bila kutumia zana

5. Pale ambapo mwajiri, chini ya kanuni ya 10 na 11 anahitajika kufanya utambuzi au tathmini ya hatari za kazi zinazohusisha ufanyaji kazi hatarishi bila kutumia zana, mwajiri anaweza kufanya utambuzi au tathmini ya hatari kwa aina za kazi kuliko utambuzi na tathmini ya hatari kwa kazi za mfanyakazi mmoja mmoja ikiwa -

(a) kazi zote za aina hiyo zinafanana; na
(b) utambuzi au tathmini ya hatari iliyofanywa kwa aina za kazi haisababishi mtu yeyote kuwekwa kwenye hatari tofauti kama tathmini ya hatari ingefanywa kwa kila kazi ya mtu mmoja mmoja.

Wajibu wa wasanifu, watengenezaji, waagizaji na wasambazaji

6.-(1) Mtu ambaye anasanifu, anatengeneza, anaingiza au anasambaza mtambo wowote kwa ajili ya matumizi mahali pa kazi atahakikisha kwamba hatari yoyote ya matatizo ya misuli na mifupa ambayo inaweza kutokea wakati mtambo unatumiwa ipasavyo mahali pa

kazi-

(a) imeondolewa; au
(b) ikiwa haiwezekani kuondoa hatari, itapunguzwa kadri inavyowezekana.

(2) Kwa madhumuni ya kanuni hii, mtambo wowote haupaswi kuchukuliwa kama unatumika ipasavyo pale unapotumika bila kuzingatia taarifa muhimu au ushauri wowote unaopatikana kuhusiana na matumizi yake.

Tathmini ya hatari

7.-(1) Mwajiri ambaye amezingatia masharti ya tathmini ya hatari chini ya kifungu cha 60 cha Sheria, atazingatia pia kanuni ya 10 na 11ya Kanuni hizi kuhusiana na kazi inayohusisha ufanyaji kazi hatarishi bila zana, endapo tathmini hiyo imezingatia hatari ya matatizo ya misuli na mifupa inayoweza kumuathiri mfanyakazi kutokana na kazi hiyo.

(2) Mwajiri atatakiwa kuzingatia masharti ya udhibiti wa hatari chini ya kanuni ya 11 ya Kanuni hizi, na iwapo hatua za kudhibiti hatari zilizopo zinadhibiti hatari ya matatizo ya misuli na mifupa inayoweza kumuathiri mfanyakazi.

(3) Pale ambapo kanuni ndogo ya (1) inatumika, mwajiri atazingatia wajibu chini ya kanuni ya 10 na kuweka kumbukumbu ya tathmini ya hatari iliyofanyika.

(4) Kanuni hii haizuii wajibu wa mwajiri kuchukua hatua za ziada za udhibiti wa hatari ya matatizo ya misuli na mifupa inayoweza kumuathiri mwajiriwa, ikiwa tathmini ya hatari au hatua za udhibiti wa hatari zilizochukuliwa hazitoshelezi.

Wajibu wa mwajiri kwa mkandarasi anayejitegemea na Majukumu mengine yanayohusiana

8. Kwa madhumuni ya kanuni hii-

(a) "mfanyakazi" inamjumuisha mkandarasi wa kujitegemea aliyepewa kazi na mwajiri na wafanyakazi wote wa mkandarasi anayejitegemea; na
(b) wajibu wa mwajiri chini ya kanuni hii umeongezwa kwa mkandarasi huyo anayejitegemea na mwajiriwa wa mkandarasi anayejitegemea, kuhusiana na masuala

ambayo mwajiri-
(i) ana udhibiti; au
(ii) angekuwa na udhibiti lakini kwa makubaliano yoyote kati ya mwajiri na mkandarasi anayejitegemea ana udhibiti bila kujali makubaliano.

Mwajiri kushauriana na mwakilishi wa afya na usalama

9. Mwajiri anapotekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Kanuni hizi atatakiwa kushauriana na wawakilishi wa afya na usalama kuhusu utambuzi, tathmini au udhibiti wa hatari za ufanyaji kazi bila kutumia zana kulingana na mazingira yatakavyokuwa.

Wajibu wa mwajiri wa kutambua kazi hatarishi zinazohusisha ufanyaji kazi bila kutumia zana

10.-(1) Mwajiri atahakikisha kwamba kazi yoyote inayofanywa, au itakayofanywa na mfanyakazi inayohusisha ufanyaji kazi hatarishi bila kutumia zana inatambuliwa.

(2) Katika Kanuni hizi "ufanyaji kazi hatarishi bila kutumia zana" unajumuisha-
(a) ufanyaji kazi bila kutumia zana wenye sifa zozote zifuatazo-
(i) matumizi ya nguvu ya kujirudia rudia au endelevu;
(ii) mkao mbaya wa kujirudia rudia au endelevu;
(iii) usogeaji unaojirudia rudia au endelevu;
(iv) matumizi ya nguvu kubwa; na
(v) kukumbwa na mitetemo endelevu.
(b) kunyanyua, kubeba au kusogeza watu au wanyama hai;
(c) kunyanyua, kubeba au kusogeza mizigo isiyo imara au isiyo na usawa au mizigo ambayo ni vigumu kushikika.

(3) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), mwajiri atahakikisha kuwa kazi yoyote inayohusisha ufanyaji kazi hatarishi bila kutumia zana inatambuliwa-
(a) kabla ya kazi yoyote inayohusisha ufanyaji kazi bila zana inafanywa kwa mara ya kwanza mahali pa kazi;
(b) kabla marekebisho yoyote hayajafanyika kwa

vitu vinavyotumika mahali pa kazi au mifumo ya kazi pamoja na kazi inayohusisha ufanyaji kazi bila zana, ikijumuisha mabadiliko ya mahali ambapo kazi hiyo inafanyika;

(c) kabla ya kitu kutumika kwa madhumuni mengine tofauti na ambayo kiliundwa ikiwa madhumuni mengine yanaweza kusababisha hatari ya ufanyaji kazi bila zana;

(d) ikiwa maelezo mapya au ya ziada kuhusu ufanyaji kazi hatarishi bila zana yanayohusishwa na kazi yamemfikia mwajiri; na

(e) ikiwa kuna taarifa imetolewa na au kwa niaba ya mfanyakazi ya uwepo wa tatizo la misuli na mifupa mahali pa kazi.

Wajibu wa mwajiri kufanya tathmini ya hatari

11.-(1) Endapo kazi inayohusisha ufanyaji kazi hatarishi bila kutumia zana umetambuliwa kwa mujibu wa kanuni ya 10, mwajiri atahakikisha kwamba tathmini inafanywa ili kubaini kama kuna hatari yoyote ya matatizo ya misuli na mifupa inayotokana na kazi hiyo.

(2) Mwajiri atahakikisha kwamba tathmini inazingatia mambo yafuatayo yanayohusiana na utekelezaji wa kazi inayotathminiwa-

(a) mikao iliyokubaliwa;

(b) usogeaji unaotumika;

(c) kiasi au kiwango cha nguvu zinazotumika;

(d) hali ya mazingira, inayojumuisha joto, baridi na mitetemo, ambayo humkumba moja kwa moja mtu anayefanya kazi; na

(e) muda wa ufanyaji kazi na muda wa urudiaji kazi.

(3) Mwajiri atahakikisha kwamba tathmini ya hatari inapitiwa upya na, inapobidi, inarekebishwa, au tathmini nyingine ya hatari inafanywa ikiwa, kutokana na hali yoyote iliyotajwa katika kanuni ndogo ya 2 (b) hadi (e) au kwa sababu nyingine yoyote, tathmini ya hatari iliyotajwa kwanza haitathmini vya kutosha hatari ya matatizo ya misuli na mifupa yanayomuathiri mfanyakazi kutokana na kazi husika.

(4) Pale ambapo tathmini ya hatari iliyofanywa kwa mujibu wa kanuni hii itabainisha kuwa kuna hatari ya matatizo ya misuli na mifupa inayomuathiri mfanyakazi, mwajiri atahakikisha kwamba mbinu zilizotumiwa kutathmini hatari na matokeo ya tathmini yanarekodiwa na kutunzwa hadi tathmini mpya ya hatari itakapohitajika kufanyika kwa mujibu wa kanuni hii au ikiwa kazi husika haitafanyika tena.

Wajibu wa mwajiri kudhibiti hatari

12.-(1) Mwajiri atahakikisha kwamba hatari yoyote ya matatizo ya misuli na mifupa inayoathiri mfanyakazi-

(a) imeondolewa; au
(b) ikiwa haiwezekani kuondoa au kupunguza hatari, vitu au utaratibu wa kazi utabadilishwa na mwajiri atahakikisha kuwepo kwa njia salama za ufanyaji kazi.

(2) Mwajiri haruhusiwi kutumia taarifa, mafunzo au maelekezo ya mbinu ya ufanyaji kazi bila kutumia zana kama njia pekee au msingi wa kudhibiti hatari isipokuwa kama njia zifuatazo za kudhibiti hatari hazitekelezeki-

(a) kuboresha-
  (i) mahali pa kazi, au hali ya mazingira, ikijumuisha joto, baridi na mtetemo, ambapo kazi inayohusisha ufanyaji kazi bila kutumia zana hufanyika; au
  (ii) mifumo ya kazi inayotumika kutekeleza kazi inayohusisha ufanyaji kazi bila kutumia zana;
(b) kubadilisha vitu vinavyotumika katika ufanyaji kazi bila kutumia
Zana; au
(c) kutumia zana saidizi.

Wajibu wa mfanyakazi

13. Mfanyakazi atashirikiana na mwajiri kuhusiana na hatua yoyote iliyochukuliwa kwa madhumuni ya kuzingatia sharti lolote lililowekwa kwa mwajiri katika kanuni za 10, 11 na 12.

Dodoma,
………………, 2023

JOYCE L. NDALICHAKO,
*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira, na Wenye Ulemavu)*

TANGAZO LA SERIKALI Na. 291 la tarehe 7/4/2023

SHERIA YA AFYA NA USALAMA MAHALI PA KAZI,

(SURA YA 297)

---

# KANUNI

---

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 109)*

KANUNI ZA UONDOAJI WA ASBESTOSI ZA MWAKA 2023

MPANGILIO WA KANUNI

*Kanuni* *Jina*

1. Jina.
2. Tafsiri.
3. Matumizi.
4. Utambuzi wa uwepo wa asbestosi.
5. Orodha ya asbestosi iliyotambuliwa.
6. Tathmini ya uwezekano wa kukumbwa na asbestosi.
7. Mpango wa usimamizi wa asbestosi.
8. Taarifa na mafunzo.
9. Uainishaji wa kazi za asbestosi.
10. Wajibu wa watu wanaoweza kukumbwa na asbestosi.
11. Udhibiti wa kukumbwa na asbestosi.
12. Kutoa taarifa ya kazi za asbestosi.
13. Majukumu ya mkandarasi aliyeidhinishwa anaefanya kazi za asbestosi.
14. Majukumu ya mamlaka ya usimamizi wa kazi za asbestosi.
15. Mahitaji ya mpango kazi wa asbestosi.
16. Eneo la asbestosi lililodhibitiwa.
17. Ufuatiliaji wa afya.
18. Vifaa kinga.
19. Kuweka lebo na alama.
20. Kumbukumbu.
21. Mazuio.

SHERIA YA AFYA NA USALAMA MAHALI PA KAZI,

(SURA YA 297)

---

# KANUNI

---

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 109)*

KANUNI ZA UONDOAJI WA ASBESTOSI ZA MWAKA 2023

Jina

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Uondoaji wa Asbestosi za Mwaka 2023.

Tafsiri

2. Katika Kanuni hizi isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"asbestosi" maana yake ni nyuzi za aina yoyote za madini ya silika zinazoweza kuingia kwenye mapafu kwa kupitia mfumo wa hewa na zisizoweza kuvunjwavunjwa, kumeng'enywa au kutolewa ndani ya mwili;

"kazi inayohusiana na asbestosi" maana yake ni kazi yoyote inayohusu kubomoa, kuondoa vitu au bidhaa zenye asbestosi;

"kifaa kinga cha kupumulia" maana yake ni kifaa ambacho huvaliwa angalau mdomoni na puani ili kuzuia kuvuta hewa yenye asbestosi;

"kikomo cha kukumbwa na asbestosi kazini" maana yake ni kikomo cha kukumbwa na asbestosi kazini cha nyuzi 0.2 za asbestosi kwa kila mililita ya hewa;

"kikomo cha muda mfupi cha kukumbwa na asbestosi " maana yake ni kiwango ambacho mfanyakazi anaweza kukumbwa na asbestosi kwa wastani wa muda usiozidi dakika kumi na tano ambacho hakipaswi kuzidishwa wakati wowote kwa siku, hata kama wastani wa kukumbwa wa masaa manne uko ndani ya kikomo cha kukumbwa kazini;

"mahali penye asbestosi" inajumuisha asbestosi yoyote iliyopo katika eneo la kazi, ikijumuisha bidhaa ya saruji ya asbestosi, ufunikaji uliotumia asbestosi, nyenzo zenye asbestosi, vumbi lenye asbestosi, bidhaa zilizofunikwa kwa asbestosi, na taka za asbestosi;

"mamlaka ya ukaguzi wa asbestosi iliyoidhinishwa" maana yake ni mtu au mkandarasi aliyeidhinishwa na Mkaguzi Mkuu kufanya kazi za asbestosi ambaye ana elimu, ujuzi na vifaa maalumu;

"mtu mwenye uwezo" maana yake ni mtu mwenye ujuzi, mafunzo na uzoefu unaohitajika kuhusiana na kazi za asbestosi na anatambuliwa na Mamlaka;

Sura ya 297

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi;

"uzuiaji kwa kutumia asbestosi" maana yake ni bidhaa yoyote ambayo ina asbestosi kwa ajili ya kuzuia joto, sauti, umeme au madhumuni mengine ikijumuisha kuzia moto isipokuwa-

(a) saruji ya asbestosi, ufunikaji kwa kutumia asbestosi;

(b) bidhaa yoyote ya lami, plastiki, au mpira ambayo ina asbestosi na sifa ya kuhimili joto au sauti tofauti na madhumuni yake kuu.

Matumizi

3. Kanuni hizi zitatumika kwa kila mwajiri, mtu aliyejiajiri na ana mfanyakazi au mtu yeyote katika eneo lenye vumbi la asbestosi.

Utambuzi wa uwepo wa asbestosi

4. Mwajiri au mtu aliyejiajiri atahakikisha kuwa -

(a) vifaa vyote vya asbestosi vilivyopo mahali pa kazi vinatambuliwa na mtu mwenye ujuzi;

(b) ikiwa hakuna uhakika wa uwepo wa asbestosi katika bidhaa, kuchukua na kupeleka sampuli ya bidhaa hiyo kuhahakikiwa na kupimwa katika maabara inayotambulika na yenye uwezo;

(c) ikiwa sehemu ya mahali pa kazi haifikiki na inadhaniwa na mtu mwenye ujuzi kuwa na

asbestosi; itatambuliwa kuwa eneo hilo lina asbestosi, na

(d) ikiwa hakuna asbestosi iliyotambuliwa mahali pa kazi kulingana na kanuni ya 4(a), (b) na (c) itathibitishwa kwa maandishi na mtu mwenye ujuzi kuwa halina asbestosi.

Orodha ya asbestosi iliyotambuliwa

5.-(1) Mwajiri au mtu aliyejiajiri atahakikisha kwamba asbestosi iliyotambuliwa au kudhaniwa kuwa ipo mahali pa kazi na mtu mwenye ujuzi kama ilivyoainishwa katika kanuni ya 4, inaingizwa katika orodha ya asbestosi ambayo itatunzwa mahali pa kazi.

(2) Orodha ya asbestosi iliyopo mahali pa kazi inatakiwa kuwa na taarifa zifuatazo:

(a) tarehe ambayo kitu chenye asbestosi kimetambuliwa;

(b) maelezo ya kitu chenye asbestosi, idadi na hali ya uchakavu;

(c) ramani yenye maelezo ya kina kuhusu maeneo yenye asbestosi;

(d) uthibitisho wa kuwepo lebo na ishara kama iilivyoainishwa katika kanuni ya 19;

(e) uainishaji wa hatari ya uwezekano wa kukumbwa na asbestosi kama ilivyofafanuliwa katika kanuni ya 6(3); na

(f) maelezo ya kazi za baadae na matukio yanayohusiana na uwezekano wa kukumbwa.

(3) Mwajiri au mtu aliyejiajiri atahakikisha kwamba mtu mwenye ujuzi anapitia na ikibidi kurekebisha orodha ya asbestosi zilizopo mahali pa kazi kwa kipindi kisichozidi miezi ishirini na nne.

(4) Orodha ya asbestosi zilizopo mahali pa kazi itarekebishwa ikiwa-

(a) vitu zaidi vyenye asbestosi vimetambuliwa; na

(b) kitu chenye asbestosi kimechakaa kwa kiasi kikubwa, kimeondolewa, kimeharibika, kimefungiwa au kufunikwa.

(5) Pale ambapo kuondolewa au ukarabati wa asbestosi umepangwa, taarifa ya kina ya orodha ya vitu

venye asbestosi vilivyopo mahali pa kazi, itafafanuliwa vya kutosha kuhusiana na kazi itakayofanywa.

(6) Mwajiri au mtu aliyejiajiri atahakikisha kwamba nakala ya orodha ya vitu vyenye asbestosi vilivyopo katika mahali pa kazi -

(a) vinatolewa kwa mkandarasi wa asbestosi aliyesajiliwa kabla ya kuanza kuondoa au kukarabati asbestosi;

(b) vitapatikana kwa urahisi kwa wafanyakazi na mkaguzi katika mahali pa kazi; na

(c) ikiwa umiliki utabadilika, apatiwe mmiliki mpya wa majengo.

(7) Mkandarasi wa asbestosi aliyesajiliwa ambaye anafanya kazi ya kuondoa au kukarabati asbestosi mahali pa kazi atahakikisha kuwa, kama kiambata kinachodhaniwa kuwepo ni asbestosi-

(a) anapata nakala ya orodha ya asbestosi kutoka kwa mwajiri au mtu aliyejiajiri; na

(b) ikiwa inadhaniwa kuwa asbestosi ipo kwenye jengo au mtambo, amjulishe mwajiri au mtu aliyejiajiri ambaye atawajibika kuhakikisha kwamba mtu mwenye ujuzi atathibitisha.

(8) Kwa kazi zote zinazofanyika mahali pa kazi ambapo kuna uwezekano wa kukumbwa na asbestosi inayopeperuka hewani-

(a) mwajiri au mtu aliyejiajiri atahakikisha kwamba mtu anayeidhinisha kazi husika anapewa nakala ya orodha ya asbestosi zilizopo mahali pa kazi;

(b) mtu anayeidhinisha kazi iliyotajwa katika aya (a), atathibitisha kutoka kwenye orodha ya asbestosi zilizopo, kama kazi zijazo na matukio yanayohusiana na uwezekano wa kukumbwa na asbestosi upo, ikijumuisha kutambua vidhibiti vinavyopendekezwa; na

(c) mwajiri au mtu aliyejiajiri atalazimika kuhakikisha kwamba vidhibiti vinavyopendekezwa vinatekelezwa kuhusiana na kazi hiyo.

(9) Asbestosi zote zilizoorodheshwa katika

orodha ya asbestosi kama inavyotakiwa na kanuni hii zitawekwa lebo, alama au ishara za wazi kwa mujibu wa kanuni ya 19.

Tathmini ya uwezekano wa kukumbwa na asbestosi

6.-(1) Mwajiri au mtu aliyejiajiri atahakikisha kwamba -

(a) tathmini ya uwezekano wa kukumbwa na asbestosi katika eneo la kazi inafanyika na Mamlaka iliyoidhinishwa ili kubaini kama mtu yeyote anaweza kuwa katika hatari ya kukumbwa; na

(b) taarifa ya tathmini iliyofanywa katika aya ya (a) itawasilishwa kwa Mkaguzi Mkuu.

(2) Mwajiri kabla ya kufanya tathmini, lazima ashauriane na kamati ya afya na usalama ili kuweka utaratibu wa kufanya tathmini ya uwezekano wa kukumbwa na asbestosi.

(3) Matokeo ya tathmini yatakuwa na uainishaji wa hatari kulingana na uwezekano wa kukumbwa kwa kila kitu chenye asbestosi, kutokana na -

(a) athari za kiafya za asbestosi;

(b) idadi ya watu wanaoweza kukumbwa katika mahali pa kazi;

(c) muda wa kuwepo katika eneo lenye asbestosi;

(d) hali ya uharibifu wa bidhaa zenye asbestosi mahali pa kazi ikijumuisha, shughuli za matengenezo, matukio yanayoweza kutokea na shughuli za kawaida mahali pa kazi; na

(e) hali ya bidhaa yenye asbestosi, ikijumuisha uchakavu.

(4) Uainishaji wa hatari unaokusudiwa katika kanuni ndogo ya (3) utatumika kubainisha iwapo kuna sababu ya kuendelea kutumia, kurekebisha au kuondolewa kwa bidhaa yenye asbestosi.

(5) Tathmini ya uwezekano wa kukumbwa, unaotokana na kazi ya kurekebisha bidhaa zenye asbestosi kama inavyotakiwa katika kanuni ndogo ya (1), (2) na (3) itajumuisha-

(a) kufafanua kila hatua ya kazi ya urekebishaji;

(b) tathmini ya hatari ya kukumbwa na asbestosi, inayohusiana na kila hatua ya kazi; na

(c) vidhibiti vinavyohitajika ili kupunguza kiwango cha hatari ya kukumbwa na asbestosi.

(6) Tathmini ya uwezekano wa kukumbwa, unaotokana na kazi ya kuondoa bidhaa zenye asbestosi kama ilivyoainishwa katika kanuni ya 16, itazingatia-

(a) vipengele vilivyofafanuliwa katika kanuni ndogo ya (5);

(b) tathmini ya hatari iliyofanywa;

(c) uwezekano wa kukumbwa kwa watu wengine ambao si wafanyakazi;

(d) uwezekano wa uchafuzi wa hewa, ardhi na maji;

(e) kuwaepusha au kuwakinga na asbetosi wafanyakazi na mahali pa kazi;

(f) usafirishaji wa bidhaa za asbestosi na taka za asbestosi; na

(g) matukio ya dharura.

(7) Mwajiri au mtu aliyejiajiri atapeleka orodha ya bidhaa zenye asbestosi na tathmini ya uwezekano wa kukumbwa katika mamlaka ya ukaguzi kwa ajili ya kupitiwa na kuidhinishwa, isipokuwa kwamba mapitio na uidhinishaji hautahitajika ikiwa kazi hiyo ilifanyika na Mamlaka ya ukaguzi.

Mpango wa usimamizi wa asbestosi

7.-(1) Pale ambapo bidhaa zenye asbestosi zinatambuliwa kama inavyotakiwa katika kanuni ya 4, mwajiri au mtu aliyejiajiri atahakikisha kuwa mpango wa usimamizi wa asbestosi mahali pa kazi unaandaliwa na mtaalamu wa asbestosi.

(2) Mpango wa usimamizi wa asbestosi utajumuisha-

(a) taratibu zinazohusiana na-

(i) utekelezaji wa kanuni ya 4, 5, 6 na 9 mahali pa kazi;

(ii) ukarabati, uondoaji na usimamizi wa bidhaa zenye asbstosi; na

(iii) utekelezaji wa Kanuni za kupiga

marufuku matumizi;

(b) utaratibu mahususi wa kupunguza hatari ya kukumbwa kwa wafanyakazi pamoja na kuathiriwa na asbestosi kwa hali zifuatazo-

(i) matukio;

(ii) dharura;

(iii) kazi ya uondoaji; na

(c) sera, utaratibu na mpango wa utekelezaji wa kuondoa bidhaa zilizopo zenye asbestosi mahali pa kazi, ambazo zinazingatia-

(i) kanuni ambayo inatekelezeka ipasavyo, na

(ii)sababu za maamuzi.

Taarifa na mafunzo

8.-(1) Mwajiri yoyote anayejihusisha na kazi zinazohusiana na asbestosi au kutumia bidhaa zenye asbestosi baada ya kushauriana na Kamati ya Afya na Usalama iliyoundwa, atalazimika kuwapa wafanyakazi taarifa na mafunzo kuhusiana na-

(a) vyanzo vya kukumbwa na asbestosi;

(b) hatari ya kiafya inayoweza kusababishwa na kukumbwa na asbestosi, ikijumuisha hatari za kiafya kwa familia za wafanyakazi na wengine, ambao wanaweza kuathirika kutokana na vifaa au nguo zilizotumika kazini kupelekwa nyumbani;

(c) tahadhari zinazopaswa kuchukuliwa na mfanyakazi kumkinga dhidi ya vihatarishi vya kiafya vinavyotokana na kukumbwa na asbestosi, ambazo zinajumuisha kuvaa na kutumia vifaa kinga;

(d) umuhimu, matumizi sahihi, matunzo na uwezo wa vifaa kinga, vifaa na hatua za udhibiti wa uhandisi zinazotolewa;

(e) tathmini ya kukumbwa na asbestosi, madhumuni ya kuchukua sampuli za hewa, umuhimu wa ufuatiliaji wa afya za wafanyakazi na faida za muda mrefu za kufanyiwa ufuatiliaji wa kiafya;

(f) muda wa kazi na kiwango cha ukomo wa kukumbwa na asbestosi;

(g) taratibu salama za ufanyaji kazi kuhusu utumiaji,

utunzaji, usindikaji, uhifadhi na utupaji wa kitu au bidhaa yoyote iliyo na asbetosi, ili kupunguza uenezaji wa asbestosi nje ya eneo la kazi; na

(h) taratibu zinazopaswa kufuatwa katika tukio la kusambaa au dharura nyingine yoyote.

(2) Mafunzo ya rejea yatatolewa juu ya masuala yanayokusudiwa katika kanuni ndogo ya (1) angalau kila mwaka au mkaguzi atakavyoelekeza.

(3) Mafunzo yatatolewa na mtu ambaye ana weledi na anayetambuliwa na Mamlaka kutoa mafunzo hayo.

(4) Mwajiri au mtu aliyejiajiri atahakikisha kwamba anatoa taarifa na maelekezo yanayohusiana na kukumbwa na madhara ya asbestosi kwa mtu yeyote katika eneo lake la kazi.

(5) Mwajiri atatoa maelekezo kwa maandishi ya taratibu zinazokusudiwa katika kanuni ndogo ya (1)(h) kwa madereva wa magari yanayobeba asbestosi au bidhaa zenye asbestosi ambayo yana uwezekano wa kusababisha uchafuzi wa mazingira au kuleta athari kwa watu.

(6) Mwajiri atatoa taarifa kwa mtu ambae anaweza kukumbwa na asbestosi katika eneo la kazi-

(a) kupitia mafunzo ya awali pale tu anapoanza ajira; na

(b) pale ambapo orodha ya bidhaa zenye asbestosi inapitiwa.

Uanishaji wa kazi za asbestosi

9.-(1) Kazi ya asbestosi daraja A-

(a) inahusisha upakaji wa saruji za asbestosi kwa namna ambayo hauhitaji maandalizi ya kwenye sakafu, na haiwezi kusababisha kusambaa kwa nyuzi za asbestosi;

(b) inahusisha uondoaji wa saruji za asbestosi isiyozidi mita kumi za mraba au mabomba yenye asbestosi au ubao pinzani wenye asbestosi; na

(c) haihitaji mkandarasi maalum wa asbestosi aliyesajiliwa.

(2) Kazi ya asbestosi daraja B-

(a) inahusisha ukarabati au ufunikaji wa bidhaa za saruji za asbestosi kwa namna ambayo hauhitaji maandalizi ya sakafuni;

(b) inahusisha kuondolewa kwa bidhaa za saruji za asbestosi au ubao pinzani wenye asbestosi; na

(c) inahitaji mkandarasi maalum wa asbestosi aliyesajiliwa.

(3) Kazi ya Asbestosi daraja C -

(a) inahusisha uondoaji, ukarabati au uwekaji wa asbestosi na bidhaa yenye asbestosi yeyote; na

(b) inahitaji mkandarasi maalum wa asbestosi aliyesajiliwa.

Wajibu wa watu wanaoweza kukumbwa na asbestosi

10.-(1) Mtu ambaye anaweza kukumbwa na asbestosi atatakiwa -

(a) kutii maagizo yanayohusu afya na usalama kazini yanayotolewa na au kwa niaba ya mwajiri;

(b) kuhudhuria mafunzo ya uelewa wa asbestosi juu ya orodha ya asbestosi zilizopo kwenye jengo; na

(c) kutoa taarifa ya bidhaa yoyote yenye asbestosi iliyoharibika kwa mwajiri au mwakilishi wa afya na usalama mahali pa kazi.

(2) Mtu ambaye anafanya matengenezo yasiyohusika na kazi za asbestosi, na ambaye anaweza kukumbwa na asbestosi atatakiwa -

(a) kupewa nakala ya orodha ya bidhaa zenye asbestosi zilizopo mahali pa kazi panapohusika ambapo matengenezo yasiyohusika na asbestosi yatafanyika;

(b) kuzuia uharibifu wa, au kusababisha usambaaji wa asbestosi mahali pakazi; na

(c) kuacha kazi mara moja na kutoa taarifa kwa mwajiri au mwakilishi wa afya na usalama mahali; pa kazi, iwapo uharibifu au usambaaji

wa asbestosi utatokea.

(3) Mtu anayefanya kazi ya asbestosi ya daraja "A" atatakiwa -

(a) kupata nakala ya orodha ya bidhaa zenye asbestosi zilizopo mahali pa kazi;
(b) kuweka mipaka ya eneo linalodhibitiwa lenye asbestosi kama inavyotakiwa katika kanuni ya 18;
(c) kutumia njia ya kuweka maji wakati wa kuondoa bidhaa zenye asbestosi;
(d) kutumia zana na vifaa vinavyofaa ili kupunguza kusambaa vumbi la asbestosi;
(e) kuhakikisha kifaa kimesafishwa baada ya kufanya kazi za asbestosi;
(f) kuhifadhi, kuweka lebo na kuondoa taka za asbestosi kwa mujibu wa kanuni ya 19; na
(g) kutumia vifaa kinga pamoja na vifaa kinga vya kupumulia vya kutupwa, na vitaondolewa kama taka za asbestosi.

(4) Mtu yeyote ambaye anahusika katika kazi ya asbestosi ya daraja B na C na ambaye anaweza kukumbwa na asbestosi mahali pa kazi, atatii maagizo yote halali yanayohusu afya na usalama mahali pa kazi, yatakayotolewa na au kwa niaba ya mwajiri au mtu aliyejiajiri, kuhusu-

(a) kutekeleza mahitaji ya mpango kazi wa asbestosi ambao umeidhinishwa kwa kazi hiyo maalum ya asbestosi, kwa mujibu wa kanuni ya 15;
(b) kutumia njia za kuweka maji wakati wa kuondoa bidhaa zenye asbestosi;
(c) kuzuia vumbi la asbestosi kusambaa kwenye hewa;
(d) aina na matumizi sahihi ya vifaa kinga;
(d) uvaaji wa kifaa cha ufuatiliaji ili kupima kiwango cha mtu kukumbwa na asbestosi;
(e) kusafisha na kuondoa taka za asbestosi;
(f) usafishaji wa mabaki ya vumbi la asbestosi linalotokana na kazi;

(g) mpangilio katika mahali pa kazi, usafi binafsi, tamaduni nzuri za mazingira, afya na usalama ikiwa ni pamoja na kula, kunywa na kuvuta sigara katika maeneo maalum yaliyotengwa;

(h) taarifa na mafunzo yaliyotolewa kama ilivyokusudiwa katika kanuni ya 8; na

(j) kuzingatia taratibu sahihi za kusafisha kama ilivyoainishwa katika mpango kazi asbestosi ulioidhinishwa.

Udhibiti wa kukumbwa na asbestosi

11.-(1) Mwajiri au mtu aliyejiajiri atahakikisha kwamba kukumbwa na asbestosi mahali pa kazi kunazuiwa au ikishindikana kudhibitiwa vya kutosha, udhibiti huo utachukuliwa kuwa wa kutosha ikiwa kiwango cha asbestosi katika hewa; -

(a) kipo chini ya kikomo cha kukumbwa kazini; au

(b) kipo juu ya kikomo, lakini sababu imetambuliwa na hatua ya haraka ya kugawa vifaa kinga vya kupumulia imechukuliwa ili kupunguza kiwango hicho.

(2) Mwajiri au mtu aliyejiajiri atadhibiti uwezekano wa mtu kukumbwa na asbestosi kwa -

(a) kupunguza au kudhibiti idadi ya watu wanaoweza kukumbwa na asbestosi;

(b) kupunguza muda ambao mtu atakumbwa au anaweza kukumbwa na asbestosi;

(c) kupunguza kiwango cha vumbi la asbestosi ambacho kinaweza kuingia katika mazingira ya kazi; na

(d) kuanzisha hatua za udhibiti wa kihandisi ili kupunguza kukumbwa na asbestosi kama-

(i) kutenganisha mchakato unaohusiana na asbestosi, kufungia bidhaa au eneo lenye asbestosi;

(ii) kuchanganya nyuzi za asbestosi na vitu vingine ili kuzuia kusambaa kwa vumbi la asbestosi;

(iii) kutumia njia ya kuweka maji kudhibiti vumbi la asbestosi pale

itakapoonekena inafaa; na

(iv) usafishaji unafanyika kwa kutumia kifaa kinachoweza kuvuta uchafu chenye ufanisi wa kuchuja wa angalau asilimia 99 ya chembe zenye ukubwa wa maikromita moja, ili vumbi lenye asbestosi lisisambae kwenye hewa ya mahali pa kazi.

(3) Pale ambapo asbestosi imeingia kwenye maji-

(a) maji yaliyochafuliwa na asbestosi kutokana na kazi iliyofanyika yatapitishwa kwenye mfumo wa kuchuja maji kabla hayajaingia kwenye mazingira; na

(b) sehemu ya mtambo wa kuchuja maji iliyotumika kuchuja asbestosi itachukuliwa kama taka ya asbestosi.

(4) Kuanzisha taratibu salama za ufanyaji kazi za maandishi ambazo mfanyakazi atatakiwa kufuata ili kuhakikisha kuwa -

(a) bidhaa zenye asbestosi zinashikwa, kuhifadhiwa, kusafirishwa na kuondolewa kwa usalama; na

(b) usimikaji, vifaa, zana na vifaa vya kuvutia uchafu vinatumiwa, vinasafishwa na kutunzwa kwa usalama.

(5) Mwajiri au mtu aliyejiajiri atatoa taarifa kwa Mkaguzi Mkuu kuhusu umwagikaji, uharibifu na usambaaji wa asbestosi ambao utakuwa ni hatarishi kwa afya za watu.

Kutoa taarifa ya kazi za asbestosi

12.-(1) Mwajiri au mtu aliyejiajiri hataruhisiwa kufanya kazi ya daraja lolote la asbestosi isipokuwa mpaka pale ambapo Mkaguzi Mkuu, amejulishwa kwa maandishi kuhusu eneo, mahali na mawasiliano ya mahali ambapo kazi ya asbestosi itafanyika siku kumi na nne kabla ya kuanza kwa kazi hiyo.

(2) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (1), Mkaguzi Mkuu anaweza kuruhusu muda mfupi zaidi wa kutoa taarifa katika hali ya dharura.

(3) Taarifa ya maandishi iandikwe kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili.

Majukumu ya mkandarasi aliyeidhinishwa kwa kazi ya asbestosi

13.-(1) Pale ambapo kazi ya asbestosi ya daraja B na C inahusika, mkandarasi aliyeidhinishwa wa asbestosi atatakiwa-

(a) kufanya aina ya kazi ya asbestosi ambayo ameidhinishwa na Mkaguzi mkuu;
(b) kuteua mwakilishi wa afya na usalama mahali pa kazi, kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 11 cha Sheria; na
(c) kupata nakala ya orodha ya bidhaa za asbestosi zilizopo kabla ya kazi ya asbesto kufanyika.

(2) Kabla ya kuanza kwa kazi yoyote ya asbestosi na wakati wa kazi hiyo, mkandarasi aliyeidhinishwa wa asbestosi atahakikisha tathmini ya hatari inafanywa ikiwa ni pamoja na-

(a) utambuzi wa vihatarishi ambavyo mtu anaweza kukumbwa;
(b) tathmini ya hatari inayohusiana na vihatarishi;
(c) hatua za kudhibiti vihatarishi vilivyopo ili kupunguza hatari;
(d) tathmini ya hatari itapitiwa -
    (i) kwa vipindi vya kawaida;
    (ii) wakati tukio limetokea; au

(iii)wakati wigo wa kazi unabadilika;

(e) kuhakikisha nakala ya tathmini ya hatari iliyohuishwa inapatikana katika eneo husika la kazi ya asbestosi.

(3) Mkandarasi wa asbestosi aliyeidhinishwa atahakikisha kwamba-

(a) mpango kazi ulioidhinishwa unawasilishwa kwa Mkaguzi Mkuu, angalau siku kumi na nne kabla ya kuanza kwa kazi ya asbestosi;

(b) anateua kwa maandishi msimamizi wa asbestosi kwa kila eneo la kazi la asbestosi, ambaye atahakikisha-

(i) uzingatiaji wa afya na usalama kwenye eneo ambalo asbestosi inaondolewa;

(ii) uzingatiaji taratibu za kuondoa au kukarabati asbestosi kwa usalama;

(iii) uzingatiaji wa matumizi sahihi ya vifaa kinga, na

(iv) usafishaji wa eneo la kazi na uondoaji wa taka.

(c) mbinu za ukarabati au kuondoa zinazohusiana na udhibiti zinazotolewa katika mpango kazi;

(d) kwamba kumbukumbu za afya na mafunzo ya wafanyakazi zinapatikana katika mahali pa kazi kwa ajili ya ukaguzi na uthibitisho;

(e) kuhakikisha kwamba taarifa za mfanyakazi zimehifadhiwa kwa muda usiopungua miaka thelathini kwa kuzingatia -

(i) anwani ya kila mradi wa kazi ya asbestosi;

(ii) majina na namba za utambulisho za wafanyakazi ambao wanaweza kukumbwa; na

(f) kabla ya kuanza kazi ya asbestosi vifaa vyote vimesafishwa na kutunzwa katika utaratibu mzuri wa kufanya kazi.

Majukumu ya mamlaka ya usimamizi wa

14. Mamlaka ya usimamizi wa kazi za asbestosi itahakikisha kwamba-

kazi za asbestosi

(a) kazi za asbestosi za daraja B na C zinafanywa na mkandarasi wa asbestosi aliyeidhinishwa;
(b) inaidhinisha mpango kazi wa asbestosi kutoka kwa mkandarasi aliyeidhinishwa;
(c) mkandarasi wa asbestosi aliyeidhinishwa kabla ya kuanza kwa kazi za asbestosi anapeleka mpango kazi kwa Mkaguzi Mkuu kwa uthibitisho;
(d) inathibitisha kumbukumbu ya mafunzo na afya za wafanyakazi wa kazi ya asbestosi;
(e) inatoa muongozo na maagizo kwa mkandarasi aliyeidhinishwa wa asbestosi kwenye mpango kazi ulioidhinishwa;
(f) inakagua uzingatiaji wa mpango kazi ulioidhinishwa na matakwa ya kanuni hizi; na
(g) inazuia mkandarasi wa asbestosi aliyeidhinishwa kutekeleza kazi ya asbestosi ambayo inahatarisha afya na usalama kwa watu hadi wakati ambapo hatari hiyo itakuwa imedhibitiwa.

Mahitaji ya mpango kazi wa asbestosi

15. Mpango kazi wa asbestosi unapaswa kuwa na

(a) jina, mawasiliano na majukumu ya mkandarasi aliyeidhinishwa wa asbestosi, kusafirisha na kutupa taka za asbestosi;
(b) jina na mawasiliano ya msimamizi wa uondoaji wa asbestosi katika eneo husika;
(c) taarifa za asbestosi inayotakiwa kuondolewa, na eneo husika, aina, kiwango na hali ya asbestosi;
(d) orodha ya majina ya wafanyakazi na namba za utambulisho na uthibitishaji wa kupatiwa mafunzo ya asbestosi na kumbukumbu za uchunguzi wa afya katika eneo la kazi ya asbestosi;
(e) tarehe ya kuanza na kukamilika kwa kazi;
(f) njia ya ufuatiliaji wa hewa inayotumiwa kwa mujibu wa kanuni ya 17;
(g) taarifa za kina za kuondoa asbestosi, vifaa na mbinu zitakazotumika na vifaa kinga sahihi vitakavyotumiwa;
(h) maelezo ya uwekaji mipaka;
(i) utaratibu wa kusafisha eneo la kazi;
(j) taratibu za dharura katika tukio la kusambaa kwa asbestosi; na
(k) njia za uondoaji taka za asbestosi.

Eneo la asbestosi lililodhibitiwa

16. Mwajiri au mtu aliyejiajiri ambaye anafanya kazi yoyote ya asbestosi-

(a) ataweka mipaka ya wazi na kutambua eneo husika; na

(b) atahakikisha kuwa hakuna mtu anayeingia au kubaki katika eneo linalodhibitiwa la asbestosi isipokuwa awe amevaa vifaa kinga vya kupumulia stahiki kama ilivyoainishwa katika kanuni ya 18.

Ufuatiliaji wa afya

17.-(1) Kila mkandarasi wa kazi ya asbestosi aliyeidhinishwa atahakikisha wafanyakazi wote wanaohusika katika kazi ya asbestosi na ambao wana uwezekano wa kukumbwa na vumbi la asbestosi, wako chini ya uangalizi wa afya na mkaguzi wa afya aliyeidhinishwa na Mkaguzi Mkuu.

(2) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (1), mkandarasi wa asbestosi aliyeidhinishwa atahakikisha kwamba mpango wa uchunguzi wa afya ulioandaliwa unatayarishwa kama masharti ya ajira, ambayo yatajumuisha-

(a) tathmini ya awali ya afya, inayofanywa na daktari aliyeidhinishwa mara tu au ndani ya siku kumi na nne baada ya mtu kuanza ajira, ambayo itajumuisha-

(i) tathmini ya historia ya afya na taaluma ya mfanyakazi;

(ii) uchunguzi wa kimwili unaofaa;

(iii) uchunguzi wa ziada ambao unapaswa kujumuisha upimaji wa utendaji kazi wa mapafu; na

(iv) uchunguzi mwingine wowote muhimu wa afya kama vile picha ya mionzi ya kifua ambayo, kwa maoni ya daktari wa afya wa mahali pa kazi aliyeidhinishwa ni muhimu ili kumwezesha daktari huyo kufanya tathmini inayofaa kwa afya.

(3) Mwajiri hataruhusu mfanyakazi ambaye amethibitishwa kuwa hatakiwi kufanya kazi za asbestosi na mkaguzi wa afya mahali pa kazi, kufanya kazi ya asbestosi:

Isipokuwa kwamba, mfanyakazi husika anaweza kuruhusiwa kurudi kazini ikiwa imeidhinishwa kwa maandishi na mkaguzi wa afya kuwa anaweza kufanya kazi hiyo.

(4) Endapo imethibitishwa kuwa mfanyakazi hatakiwi kufanya kazi ya asbestosi kama ilivyoainishwa katika kanuni ndogo ya (4) kutokana na kuathiriwa na asbestosi, mwajiri atafanya uchunguzi wa tukio hilo.

(5) Kutoa taarifa ya matukio na ugonjwa kwa Mkaguzi Mkuu na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi kunazingatiwa kama ilivyoainishwa.

Vifaa kinga

18.-(1) Pale ambapo vifaa kinga vya kupumulia vimetolewa, mwajiri au mtu aliyejiajiri atahakikisha kwamba -

(a) kifaa husika kina uwezo wa kuweka kiwango cha kukumbwa na asbestosi chini ya kikomo cha kukumbwa mahali pa kazi;
(b) kifaa husika kinatumika, kinahifadhiwa na kutunzwa kwa usahihi na ipasavyo;
(c) taarifa, maelekezo, mafunzo na usimamizi ambao ni muhimu kuhusiana na matumizi ya kifaa kinga, yanatolewa kwa watu; na
(d) kifaa kinawekwa katika hali nzuri na utaratibu mzuri wa kufanya kazi.

(2) Mwajiri au mtu aliyejiajiri atatakiwa -

(a) kutotoa kinga kwa mtu, isipokuwa pale ambapo kifaa hicho kimesafishwa na kimetakaswa; na
(b) kuwa na sehemu ya kuhifadhia vifaa kinga wakati ambapo havitumiki.

(3) Mwajiri au mtu aliyejiajiri atahakikisha kwamba, vifaa kinga vyote vilivyochafuliwa na vumbi la asbestosi vinasafishwa kwa uangalifu na-

(a) endapo vifaa kinga vinasafishwa kwenye eneo la kazi, tahadhari zitachukuliwa ili kuzuia uchafuzi wa eneo wakati wa kusafisha;
(b) maji ambayo yametumika kusafisha eneo la kazi yanaondolewa kwa njia ya kuzuia

uchafuzi wa mazingira; na

(c) maji ambayo yametumika kusafisha vifaa yatachujwa kwa mujibu wa kanuni ya 11(3) kabla ya kutolewa kwenye mfumo wowote wa maji.

(4) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (3)(a), mwajiri au mtu aliyejiajiri atahakikisha kwamba hakuna mtu anatoa vifaa kinga vichafu kutoka mahali pa kazi.

Kuweka lebo na alama

19.-(1) Asbestosi zote zilizo kwenye orodha mahali pa kazi, kama inavyotakiwa na kanuni ya 4 na 5, zitatambuliwa kwa uwazi kwa kutumia alama ya picha iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

(2) Taka zote za asbestosi zitawekwa lebo kama iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

(3) Sehemu ya ardhi iliyochafuliwa na taka za asbestosi, zitawekwa wazi na kuwekwa alama kwa kutumia lebo ya onyo iliyoainishwa katika Jedwali la Tatu.

Kumbukumbu

20. Mwajiri atatakiwa -

(a) kutunza kumbukumbu za orodha zote za asbestosi zilizopo, tathmini za uwezekano wa kukumbwa, taarifa za ufuatiliaji wa afya, na taarifa na mafunzo yaliyotolewa mahali pa kazi;

(b) kwa kuzingatia kanuni ya 20(c), kuhakikisha kumbukumbu kama ilivyoainishwa katika kanuni 20(a) apewe mkaguzi, isipokuwa kwamba kumbukumbu za afya za mtu binafsi, hatopewa bila kibali cha maandishi kutoka kwa mfanyakazi husika;

(c) kuhakikisha kumbukumbu za tathmini zote na orodha ya asbestosi zilizopo mahali pa kazi zinapatikana kwa ajili ya kusomwa na mwakilishi wa afya na usalama au kamati husika ya afya na usalama; na

(d) kutunza kumbukumbu zote zilizotajwa katika kanuni ya 20(a) kwa muda usiopungua miaka thelathini.

Mazuio

21. Mtu hataruhusiwa -

(a) kuuza, kutoa msaada, kutumia tena, kuirudisha katika matumizi asbestosi aubidhaa yenye asbestosi;

(b) kuhifadhi kwa muda asbestosi au bidhaa yenye asbestosi kwa muda zaidi ya miezi 3 kabla ya uondoaji;

(c) kuhifadhi kwa muda bidhaa yenye asbestosi iliyokusudiwa kutupwa kwa njia ambayo inaweza kuchafua ardhi au mifumo ya maji, au inaweza kusababisha kusambaa kwa vumbi la asbestosi;

(d) kutumia au kuruhusu matumizi ya hewa iliyo gandamizwa ili kuondoa vumbi la asbestosi kutoka kwenye sakafu au mtu;

(e) kutumia zana za nguvu ya umeme kukata, kusaga au kutoboa bidhaa yenye asbestosi;

(f) kuvuta sigara, kula, kunywa au kuweka chakula au vinywaji katika eneo linalodhibitiwa la asbestosi; na

(g) kusafisha au kutayarisha sakafu ya saruji yenye asbestosi kwa-

(i) kusafisha kwa maji yenye mgandamizo mkubwa;

(ii) kusafisha kwa kemikali;

(iii)kukwangua kwa maji au njia kavu;

(iv)kusugua kwa maji au njia kavu; na

(v) njia nyingine yoyote ya kusafisha au kuandaa sakafu.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 19(1)(2))*

ALAMA YA ASBESTOSI



HATARI: ASBESTOSI
INAWEZA KUSABABISHA SARATANI

<u>ASBESTOSI</u>
HATARI INAWEZA KUSABABISHA SARATANI KWA KUVUTA PUMZI

Usishughulike kufanya lolote kwenye eneo hili hadi tahadhari zote zilizoelekezwa katika Kanuni za Uondoajiwa Asbestosi na Karatasi ya Maelezo ya Usalama isomwe na kueleweka.

Usivute vumbi. vaa kifaa cha kufunika uso cha kupumulia.

Zingatia Kanuni za Upunguzaji wa Asbestosi zilizobainishwa katika vipengele vya kuzuia.

Wakati wa kuoga, ondoa glavu na ovaroli za kutupwa kabla ya kuondoa kifaa cha kupumulia.

Tupa taka za asbestosi, kwa kuzingatia Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191.

## JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 12(3))*

## FOMU YA TAARIFA YA JUMLA YA KAZI INAYOHUSISHA ASBESTOSI

(Fomu hii inatakiwa iwasilishwe kwa Mkaguzi Mkuu siku kumi na nne kabla ya kuanza kwa kazi hiyo)

A. Kwa Matumizi Rasmi tu

| | |
|---|---|
| Namba ya Usajili Mahali pa Kazi | |
| Namba ya Taarifa | |

B. Ikamilishwe na Mtu anayetoa taarifa:

1. Taarifa za Mawasiliano

<table>
<tr><td colspan="3">Tarehe ya Taarifa</td><td>Jina la Mkandarasi wa Asbestosi</td></tr>
<tr><td colspan="3">Jina la Mteja:</td><td rowspan="2"></td></tr>
<tr><td colspan="3"></td></tr>
<tr><td colspan="3">Taarifa za Mawasiliano ya Mteja:</td><td>Taarifa za Mawasiliano ya Mkandarasi:</td></tr>
<tr><td>Anuani ya Makazi</td><td>Sanduku la Posta</td><td>Simu/Barua Pepe</td><td rowspan="2"></td></tr>
<tr><td></td><td></td><td></td></tr>
<tr><td colspan="4">Mahali pa Kazi ya Asbestosi:</td></tr>
</table>

2. Maelezo ya Shughuli Zinazopaswa Kufanyika

<table>
<tr><td>Tarehe ya kuanza:</td><td></td></tr>
<tr><td>Tarehe ya kukamilisha:</td><td></td></tr>
<tr><td>Idadi ya wafanyakazi:</td><td></td></tr>
<tr><td>Kiasi cha asbestosi kinachoweza kuhusika:</td><td></td></tr>
<tr><td>Mahali asbestosi ilipo:</td><td></td></tr>
<tr><td>Kazi za asbestosi zinazohusika (kwa mfano, kuondolewa, kutengeneza, kufungia, nk)</td><td></td></tr>
<tr><td>Njia ya kutumia kukandamiza vumbi (kwa mfano, kumwagia maji, kuvuta vumbi)</td><td></td></tr>
<tr><td colspan="2">Maelezo mafupi ya kazi inayopaswa kufanywa (ambatanisha nakala ya mpango wa kazi na Mchoro wa eneo):</td></tr>
</table>

JEDWALI LA TATU

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 19(3))*

Mahitaji ya Kuweka Lebo kwa Taka za Asbestosi

A. Sampuli ya Lebo ya Eneo Lililochafuliwa

| |
|---|
| ONYO |
| Ina Nyuzi za Asbestosi<br>Epuka Kutengeneza Vumbi<br>Ugonjwa wa Mapafu na Hatari ya Saratani<br>Vifaa vya Kupumulia na Mavazi ya Kinga Vinahitajika Katika Eneo Hili |

B. Sampuli ya Ishara ya Onyo kwa Eneo Linalodhibitiwa

| |
|---|
| ONYO |
| Asbestosi<br>Ugonjwa wa Mapafu na Hatari ya Saratani<br>Wafanyakazi Walioidhinishwa Pekee!<br>Vif aa vya Kupumulia na Mavazi ya Kinga Vinahitajika Katika Eneo Hili |

Dodoma,
3 Aprili, 2023

JOYCE L. NDALICHAKO,
*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu*
*(Kazi, Vijana, Ajira, na Wenye Ulemavu)*

TANGAZO LA SERIKALI Na. 292 la tarehe 7/4/2023

SHERIA YA AFYA NA USALAMA MAHALA PA KAZI,

(SURA YA 297)

## KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 109)*

KANUNI ZA VIFAA KINGA ZA MWAKA 2023

MPANGILIO WA KANUNI

*Kanuni* *Jina*


1. Jina.
2. Tafsiri.
3. Matumizi.
4. Utoaji wa vifaa kinga.
5. Vifaa kinga sahihi na madhubuti.
6. Tathmini ya kifaa kinga.
7. Utunzaji na ubadilishaji wa kifaa kinga.
8. Uhifadhi wa kifaa kinga.
9. Taarifa, maelekezo na mafunzo.
10. Matumizi ya kifaa kinga.
11. Utoaji wa taarifa ya upotevu au uharibifu.
12. Uthibitisho wa ubora wa vifaa kinga.
13. Vifaa kinga dhidi ya kemikali na visababishi vya muwasho.

SHERIA YA AFYA NA USALAMA MAHALA PA KAZI,

(SURA YA 297)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 109)*

KANUNI ZA VIFAA KINGA ZA MWAKA 2023

Jina

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Vifaa Kinga za Mwaka 2023.

Tafsiri

2. Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo:-

"egonomia" maana yake ni muingiliano sahihi unaozingatia mahitaji ya kimaumbile na kiutambuzi ya mtu na mazingira anayoishi au kufanyia kazi;

"kifaa kinga" maana yake ni kifaa chochote kilichotengenezwa kwa ajili ya kuvaliwa au kutumika na mtu kwa ajili ya kumlinda dhidi ya kihatarishi kimoja au zaidi cha afya na usalama, ambacho:-

(a) kimetengenezwa na vitu kadhaa ambavyo vimeunganishwa kikamilifu na mtengenezaji kwa ajili ya kumlinda mtu dhidi ya hatari moja au zaidi zinazoweza kutokea kwa wakati mmoja;

(b) kinaweza kuvaliwa chenyewe au kuvaliwa pamoja na visivyo vifaa kinga kwa ajili ya kufanya kazi fulani; na

(c) kinaweza kuwa na kitu au sehemu ambayo inaweza kubadilishwa kwa ajili ya ufanisi wa kifaa hicho;

"Mamlaka" maana ni Mamlaka ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi.

Matumizi

3.-(1) Kanuni hizi zitatumika katika maeneo yote ya kazi kama ilivyoelezwa katika Sheria.

(2) Kanuni ya 4 hadi ya 12 hazitatumika kuhusiana na vifaa kinga ambavyo ni-

(a) nguo za kawaida na sare ambazo hazilindi afya na usalama wa mvaaji;

(b) vifaa vinavyobebeka vya kugundua na kuashiria hatari; na

(c) vifaa vinavyotumika wakati wa michezo.

(3) Kifaa kinga chochote cha kichwa kinachotolewa kwa mujibu wa Kanuni hizi kitazingatia Sheria au amri nyingine yoyote ambayo inatekeleza masharti yoyote ya usanifu au utengenezaji kuhusiana na afya au usalama katika sekta husika.

Utoaji wa vifaa kinga

4.-(1) Kila mwajiri atahakikisha anawapatia vifaa kinga stahiki wafanyakazi ambao wanaweza kuwa katika hatari za kiafya na kiusalama kazini isipokuwa pale ambapo hatari hiyo imedhibitiwa vya kutosha kwa njia nyinginezo.

(2) Mtu aliyejiajiri atahakikisha kuwa anatumia kifaa kinga sahihi akiwa katika hatari ya kiafya au kiusalama kazini isipokuwa pale ambapo hatari hiyo imedhibitiwa vya kutosha kwa njia nyinginezo.

(3) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1) na (2) kifaa kinga hakitakuwa sahihi isipokuwa kama kinafaa kutumika kujikinga na hatari zilizopo katika eneo la kazi na hali hatarishi ambayo wafanyakazi wanaweza kukumbana nayo ikiwa-

(a) kinazingatia mahitaji ya egonomia na hali ya afya ya mtu au watu ambao watakitumia;

(b) kina uwezo wa kumtosha mtumiaji kwa usahihi, kama kuna ulazima wakufanya marekebisho, yazingatie wigo wa uhitaji kulingana na muundo wa kifaa;

(c) kwa kadri inavyowezekana, kinaufanisi wa kuzuia au kudhibiti hatari bila kuongeza hatari zaidi; na

(d) kinazingatia sheria yoyote ambayo inatekelezwa chini ya masharti ya muundo au utengenezaji kulingana na afya au usalama wa kifaa kinga.

Vifaa kinga sahihi na madhubuti

5.-(1) Kila Mwajiri atahakikisha kuwa, endapo kuna hatari zaidi ya moja kwa afya au usalama, mfanyakazi wake

anavaa au kutumia kwa wakati mmoja kifaa kinga zaidi ya kimoja, na kuhakikisha kuwa kifaa hicho kinaendana na kinaendelea kuwa na ufanisi dhidi ya hatari zinazohusika.

(2) Kila mtu aliyejiajiri atahakikisha kuwa, endapo kuna hatari zaidi ya moja kwa afya au usalama, anavaa au kutumia kwa wakati mmoja zaidi ya kifaa kinga kimoja, na atahakikisha kifaa hicho kinaendana na kinaendelea kuwa na ufanisi dhidi ya hatari zinazohusika.

Tathmini ya kifaa kinga

6.-(1) Kabla ya kuchagua kifaa kinga chochote kwa mujibu wa kanuni ya 4, mwajiri atahakikisha kwamba mapendekezo muhimu ya mwakilishi wa afya na usalama au kamati ya afya na usalama na afisa usalama yanazingatiwa.

(2) Mwajiri au mtu aliyejiajiri atahakikisha kuwa tathmini inafanywa ili kubaini kama kifaa kinga kinafaa.

(3) Tathmini inayotakiwa na kanuni ndogo ya (2) itajumuisha -

(a) tathmini ya hatari yoyote au hatari kwa afya au usalama ambayo haiepukiki kwa njia nyingine;

(b) ufafanuzi wa sifa ambazo lazima kifaa kinga kiwe nazo ili kiwe na ufanisi dhidi ya hatari zilizotajwa katika kanuni ndogo ya 3(a), na kwa kuzingatia hatari zozote ambazo kifaa chenyewe kinaweza kusababisha; na

(c) ulinganisho wa sifa za vifaa kinga vilivyopo na sifa zilizotajwa katika kanuni ndogo ya (3)(b).

(4) Kila mwajiri au mtu aliyejiajiri anayetajwa na kanuni ndogo ya (1) atahakikisha tathmini inafanywa, inapitiwa na mabadiliko yanazingatiwa iwapo:-

(a) kuna sababu ya kudhaniwa kuwa hakifai; au

(b) kumekuwa na mabadiliko makubwa katika kazi ambayo kinahusiana nayo.

Utunzaji na ubadilishaji wa kifaa kinga

7.- (1) Kila mwajiri atahakikisha kwamba kifaa chochote cha kujikinga kinachotolewa kwa wafanyakazi wake kinatunzwa, kinabadilishwa, kinakarabatiwa au kusafishwa ili kifanye kazi iliyokusudiwa kwa ufanisi.

(2) Kila mtu aliyejiajiri atahakikisha kwamba kifaa

chochote cha kujikinga anachokitumia anakitunza, anakibadilisha, anakikarabati au anakisafisha ili kifanye kazi iliyokusudiwa kwa ufanisi.

(3) Kila mwajiri au mtu aliyejiajiri atahakikisha kwamba kifaa kinga chochote ambacho kimethibitika kuwa hakiwezi kutunzwa, kukarabatiwa au kusafishwa hakitumiki.

Uhifadhi wa kifaa kinga

8. Pale ambapo mwajiri au mtu aliyejiajiri anahitajika, kwa mujibu wa kanuni ya 4, atahakikisha anatoa au anatumia vifaa kinga, pia atahakikisha uhifadhi unaofaa wa vifaa hivyo wakati havitumiki.

Taarifa, maelekezo na mafunzo

9.-(1) Pale ambapo mwajiri anatakiwa kuhakikisha vifaa kinga vinatolewa kwa mwajiriwa, atahakikisha kwamba mfanyakazi anapewa taarifa, maelekezo na mafunzo ambayo yatajumuisha -

(a) hatari ambazo kifaa kinga kitaepusha au kupunguza na mipaka ya matumizi;

(b) wafanyakazi wanaelekezwa na kufunzwa jinsi ya kuvitumia, kuvisafisha na kuvitunza;

(c) madhumuni na namna ambayo kifaa kinga kitatumika; na

(d) hatua za kuchukuliwa na mfanyakazi ili kuhakikisha kuwa kifaa kinabaki katika hali ya ufanisi na kufanya kazi iliyokusudiwa kama inavyoelekezwa na kanuni ya 7(1).

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), taarifa na maelekezo yanayotolewa kwa mujibu wa kanuni hiyo hayatatosheleza na kufaa isipokuwa kama yataeleweka kwa watu waliokusudiwa.

Matumizi ya kifaa kinga

10.-(1) Mwajiri atachukua hatua zote zinazofaa ili kuhakikisha kifaa kinga kinachotolewa kwa wafanyakazi wake kwa mujibu wa kanuni ya 4(1) kinatumika ipasavyo.

(2) Mfanyakazi atatumia kifaa kinga chochote alichopewa kwa mujibu wa kanuni hizi kulingana na mafunzo na maelekezo ya matumizi ya kifaa kinga alichopatiwa kwa mujibu wa kanuni ya 9.

(3) Mtu aliyejiajiri atatumia kikamilifu na ipasavyo

kifaa kinga chochote kwa mujibu wa kanuni ya 4(2).

(4) Mfanyakazi na mtu aliyejiajiri ambaye amepewa kifaa kinga kwa mujibu wa kanuni ya 4 atachukua hatua zote zinazofaa ili kuhakikisha kinarejeshwa mahali maalum pa kuhifadhia baada ya matumizi.

(5) Kazi ambayo inachukua muda mfupi au mfanyakazi ana uzoefu nayo kwa muda mrefu na haijawahi kusababisha ajali haitazuia matumizi ya vifaa kinga.

(6) Mwajiri au mtu aliyejiajiri atatumia vifaa kinga kama suluhisho la mwisho la kinga dhidi ya hatari.

Utoaji wa taarifa ya upotevu au uharibifu

11. Mfanyakazi ambaye amepewa kifaa kinga kwa mujibu wa kanuni ya 4(1) atatoa taarifa ya upotevu au uharibifu wa kifaa hicho mara moja kwa mwajiri wake mara baada ya kupotea au kuharibika.

Uthibitisho wa ubora wa vifaa kinga

12.-(1) Itakuwa ni wajibu wa kila mtu ambaye, anasanifu, anatengeneza, anaingiza au anasambaza vifaa kinga, kukusanya taarifa na kuwasilisha nyaraka za kitaalamu kwa mamlaka husika kuhusu matumizi ya kifaa yaliyokusudiwa, kujaribiwa na kuidhinishwa na kuhusu hali yoyote ya muhimu ili kuhakikisha matumizi sahihi kwa ajili ya kulinda usalama wa wafanyakazi.

(2) Uwasilishaji wa nyaraka za kitaalamu kama ilivyo katika kanuni ndogo ya (1) hautahitajika kwa mazingira ya aina ya kifaa kinga chenye usanifu rahisi ambapo msanifu anadhani mtumiaji atatathmini viwango vya uzuiaji wa hatari ndogo ambapo madhara yake yanaweza kutambuliwa na mtumiaji kadiri ya muda.

Vifaa kinga dhidi ya kemikali na visababishi vya muwasho

13.Itakuwa ni wajibu wa mwajiri kuwapatia wafanyakazi -

(a) vifaa kinga vya kupumulia vinavyofunika mwili mzima kwa ajili ya kumlinda mfanyakazi dhidi ya mazingira ya kazi yenye viambata vya sumu;
(b) vifaa kinga vya kupumulia vinavyofunika mwili mzima kwa ajili ya kumlinda mfanyakazi dhidi ya mazingira ya kazi yenye viambata vya sumu;
(c) vifaa kinga vinavyomlinda mfanyakazi dhidi ya

madhara ya kemikali au mionzi ayonishi; na

(d) vifaa kinga vya dharura kwa ajili ya matumizi katika mazingira ya joto la juu ambalo madhara yake yanalinganishwa na yale ya joto la hewa la $100^0$C au zaidi na ambalo linaweza kuwa au lisiwe na sifa ya kuwepo kwa mionzi isiyo ayonisha, miale ya moto au kumwagika kwa kiasi kikubwa cha vitu vinavyoyeyuka.

Dodoma,
3 Aprili, 2023

JOYCE L. NDALICHAKO,
*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu*
*(Kazi, Vijana, Ajira, na*
*Wenye Ulemavu)*